# MUUNDO WA CHAMA

Taqiuddin An-Nabahani

Hizb ut Tahrir

**Chapa ya Uhariri wa 1440H / 2019M**

**Muundo wa Chama**

Kutoka karne ya 13 Hijria (karne ya 19 Miladi) zilisimama harakati nyingi za kutaka kuleta muamko lakini zikafanya majaribio ambayo hayakufaulu licha ya kwamba ziliacha athari kubwa kwa watakaokuja baada yao ili (na wao) kufanya tena majaribio.

Mwenye kufuatilia majaribio haya na mwenye kuzisoma harakati hizi ataona kwamba sababu msingi ya kutofaulu harakati hizi zinarudia katika upande wa muundo (wao) katika mambo manne:

1. Zilikuwa zimebuniwa juu ya fikra jumla zisizokuwa na shabaha maalum kiasi kuwa ikawa yakaribia kutokuwa wazi au kutofahamika kabisa licha ya kwamba zilikuwa zimepoteza usafi na uwazi.

2. Hawakufahamu twariqa (njia) ya kutekeleza fikra zao bali zikawa zinakwenda kwa mbinu za kiholela (kubahatisha) na kombo licha ya kuwa zilikuwa zimeghubikwa na kufichika na kutokuwa wazi.

3. Zilikuwa zikitegemea watu ambao wao wenyewe ufahamu wao hauja kamilika na kuwa sahihi na hawakuwa na nia thabiti bali walikuwa na raghba na hamasa tu.

4. Watu waliochukuwa majukumu ya harakati (hizi) hawakuwa na fungamano sahihi kati yao bali ni muundo wa chama (kiholela) tu ulioishia kupeana majukumu na kazi na kupeana majina ya vyeo.

Hivyo haikuwa ajabu kwa harakati hizi kutumia nguvu na hamasa na juhudi zake mpaka zikamalizika kisha zikazorota na kusambaratika halafu zikazuka harakati nyingine za watu wengine wakipita humo humo mpaka na wao wakamaliza akiba ya juhudi zao na wakaishia walipoanzia wenzao. Kwa hivyo, ilikuwa ni jambo la kimaumbile (kutarajiwa) kwa vikundi

hivi kuporomoka na kumalizika hazina ya juhudi na hamasa walizokuwa nazo mpaka wakaishiwa, na harakati zao zikapotea na kusambaratika. Na zikasimama baada yao harakati nyingine za watu wengine wakifanya mzunguko huo huo mpaka na wao wakaishiwa na hazina ya juhudi zao na hamasa zao katika kiwango fulani, na ikawa ndio hivyo hivyo na kuendelea. Kuporomoka kwa harakati hizi lilikua ni jambo la kutarajiwa kwa sababu hazikusimama juu ya fikra sahihi iliyo wazi na kuwa na malengo fafanuzi na wala hazikujua twariqa (njia) iliyonyooka na wasimamizi wa harakati hizi wao wenyewe walikuwa si wakomavu wa kifikra na fungamano lao halikuwa sahihi.

Ama kuhusu fikra na twariqa (njia) ya harakati hizi zilikuwa za makossa kwa sababu zilikuwa zimesimama juu ya falsafa au fikra za makosa (lau zilikuwepo). Baadhi ya harakati hizi zilikuwepo za Kiislamu na zilikuwepo za kitaifa; wasimamizi wa harakati hizi za Kiislamu walikuwa wakilingania Uislamu kwa sura ya kiholela bila ya miiko (kuzuiya kuingia fikra ngeni) na walijaribu kupindisha maana ya Uislamu (ta'awiil) ili Uislamu uafikiane na dhurufu zilizokuwepo wakati huo. Au upindishaji huo uwe ni udhuru kubakia na misimamo waliokwisha kuichukuwa au mipya watakayoichukuwa ambayo si ya Kiislamu. .

Amma waliosimama juu ya harakati za kitaifa walikuwa ni baadhi ya waarabu wakilingania kuleta mwamko wa waarabu kwa msingi wa utaifa usiokuwa wazi na kufahamika, tena pasina kujali Uislamu na Waislamu. Walikuwa wakitegemea sana (kuwavuta watu) kwa maneno ya usisi, heshima, utukufu, waarabu, uarabu, uhuru na yanayofanana na hayo. Pasina maneno haya kuwa na ufahamu wowote ulio wazi kwao wao na unao afikiana na uhakika wa mwamko. Na walikuwa baadhi ya waturuki wakilingania kusimamishwa mwamko wa kizalendo wa kituruki kwa msingi wa utaifa. Wote hao waarabu na waturuki walikuwa wakitumika na mkoloni ambaye pia alikuwa anaendesha kampeni kama hizo katika nchi za Balkan. Kwa lengo la kuzitenganisha kutoka serikali ya kiuthmani ambayo ndio iliyokua serikali ya Kiislamu.

Kulizushwa mijadala mikubwa isiyokuwa na faida na kutupiana maneno baina ya watu wa harakati mbili za Kiislamu na za kitaifa katika magazeti na majarida, mwisho wa mijadala hii ilikua: Je ni ipi harakati bora na ya kufaa zaidi baina ya jumuiya za kiarabu au za Kiislamu? Ukapotezwa muda mrefu na juhudi ikatumiwa ndani yake isiyokuwa na natija kwani zote hizi (harakati za) umoja wa kiarabu na umoja wa Kiislamu zilikuwa hazina ukweli licha ya kwamba zilikuwa ni mipango ya kikoloni kulaza akili za Waislamu juu ya serikali ya Kiislamu. Kwa hivyo, haikuishia kwa kupoteza juhudi kwa kutokuwa na natija tu, bali zikavuka mipaka kwa kuwekwa mbali serikali ya Kiislamu machoni na akilini mwa Waislamu.

Sambamba na harakati za Kiislamu na harakati za kitaifa zikazuka harakati za kizalendo katika miji tofauti tofauti ya Kiislamu ikiwa ni matokeo ya makafiri wakoloni kuzichukua sehemu za serikali ya Kiislamu na natija ya dhulma za kisiasa na kiuchumi zilizo wakumba watu kwa sababu ya kutawalishiwa mfumo wa kibepari, licha ya kwamba harakati hizi ziliripuka kutokana na machungu, zipo zilizobakia na hisia za Kiislamu na nyengine zilifuta kabisa na kubakisha uzalendo tu. Kwani mkoloni ndiye aliyekuwa akizidhibiti. Na katika mazingira hayo zikaripuka kizalendo na kuushughulisha Ummah kwa mapambano yasiyo na faida yaliyompa nguvu mkoloni, ukiongezea na kutokuwa kwao na fikra nzuri . Kwa sababu ya athari ya harakati pandikizi ambazo alikua akizisimamia mkoloni, kutokana na msukumo huu wa kizalendo zikajitosa uwanjani kushughulisha Ummah kwa mapambano ya kipuzi ambayo yalimuimarisha adui licha ya kwamba zilikua harakati na mapungufu ya kifikra itakayo ziongoza harakati hizi.

Sisi tunaamini kwamba muono sahihi wa mabadiliko ya kweli kuweza kuleta mwamko ni mfumo unaojumuisha fikra na njia viungane kwa pamoja, na kwamba mfumo huu ni

Uislamu kwa sababu ni aqida inayotoa nidhamu ya mambo yote ya kiserikali na Ummah na utatuzi wa kila tatizo maishani.

Licha ya kuwa Uislamu ni mfumo wa kiulimwengu, lakini sio katika njia yake kuanza kufanya kazi kiulimwengu unaposimama bali (utaanza eneo moja kisha isambae maeneo mengine). Bali hakuna budi ulinganizi uwe wa kiulimwengu na kuteuliwe maeneo malumu ima eneo moja au maeneo kadhaa isimame hapo dola ya Kiislamu na kumakinika na isambae usambaaji wa kimaumbile itakusanya miji ya Kiislamu kwanza mpaka kisha itaubeba Uislamu kuupeleka maeneo yaliyo bakia ulimwenguni.

Ulimwengu mzima ni pahala penye kufaa kwa ulinganizi wa Kiislamu lakini kwa sababu watu wa biladi za Kiislamu wanauamini Uislamu hakuna budi kuanza ulinganizi ndani yake. Na kwa kuwa miji ya Kiarabu watu wake wanazungumza Kiarabu, na lugha ya kiarabu ni kiungo msingi cha Uislamu na sehemu ya thaqafa ya Kiislamu, imekuwa ni bora zaidi kuanza kubeba ulinganizi huu katika miji ya kiarabu. Na hapana budi kuchanganya nishati na nguvu ya lugha ya kiarabu na nguvu ya Uislamu ili kuunganisha pamoja lugha ya kiarabu na Uislamu kwa sababu ya nguvu na athari kubwa zinazopatikana ndani yake (kiarabu na Uislamu) kwa kuweza kuathiri, kupanuka na kuenea.

Kwa hivyo, yatarajiwa kuanza serikali ya Kiislamu katika biladi za kiarabu itakayokua kiini cha serikali ya Kiislamu itakayokusanya biladi zote za Kiislamu. Pamoja na kuwa ni lazima ulinganiwe Uislamu katika biladi za kiarabu, lakini pia ni lazima hivyo hivyo utumwe ulinganizi kwa biladi zote za Kiislamu zilizobakia. Sio maana ya kuanzia kazi katika biladi za kiarabu kwamba haifanywi kazi kwengine mpaka itimie kuziunganisha chini ya serikali ya Kiislamu, bali hufanywa kazi katika biladi za kiarabu ili kusimamisha serikali ya Kiislamu kisha serikali ipanuke kwa kuanza na maeneo ya karibu yanayopakana nayo, kisha iendelee kupanuka pasina kujali kuwa ni biladi ya kiarabu au isiyokuwa ya kiarabu.

Tumesema kwamba mtazamo wa kweli wa mwamko ni mfumo unaojumuisha fikra na twariqa pamoja. Na hakuna budi ila kufahamu hayo mawili kwa kila kikundi kinacholenga kutekeleza kazi yake kwa dhati zitakazoweza kuleta mwamko.

Mfumo huu umeshakuwa wazi na kwa sasa umeshafahamika kwa kikundi ambacho kinataka kupiga hatua kusonga mbele. Basi ni jambo la kimaumbile baada ya ufafanuzi huo wa mfumo, kikundi kitakachopata ufahamu huu ni kikundi chenye athari nzuri, chenye kupiga hatua, chenye kusonga mbele na chenye kupendwa na kulindwa na mujtama na kubeba majukumu yake, kwa sababu ni kikundi kilichobobea fikra zake, chenye ufahamu safi na makini na njia yake na chenye kufahamu lipi suala/kadhia nyeti.

Lakini si tu kikundi kikipata ufahamu mzuri imetosheleza kufikia mwamko sahihi, isipokuwa watakapo patikana watu wenye kufaa kwenye kundi hili, na liwe fungamano la hao watu ni fungamanao sahihi linalozaa natija na liwe kwa mujibu wa fungamano la kichama lenye kuamua kufaa kwa watu hao.

Chama cha kimfumo hufanya twariqa ya fungamano katika kikundi chake ni kuiamini aqida na ukomavu katika thaqafa ya kichama. Kwa hivyo, uamuzi wa kufaa kwa watu huwa ni wa kimaumbile kwa kuyeyuka kwao katika chama pindi ulinganizi unapoingiliana nao. Basi itakuwa kinachoamua kufaa kwao ni twariqa ya mafungamano sio kamati ya chama, kwa sababu fungamano linalo wafungamanisha watu hawa katika chama ni aqida na thaqafa ya kichama inayo tokamana na aqida hiyo

Tukichunguza vikundi vilivyowahi kuwepo katika harakati zilizojitokeza katika karne ya 19 iliyopita, tunaona kwamba twariqa/njia ya kuunda vyama vyao ilikuwa mbovu ikawa ni

sababu msingi ya kuporomoka kwao, kwa sababu havikuundwa juu ya msingi wa kichama/kihizb. Bali vilisimama juu ya msingi wa kijumuiya au chama kijina.

Hii ni kwa sababu Waislamu kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia walijua wanayo serikali ya Kiislamu. Pamoja na udhaifu wa serikali hiyo na kudhoofika kwake, na tofauti ya mitazamo juu yake. Licha ya hayo serikali ilibakia kuwa ndio tegemeo lao kififikra na kimtazamo. Waarabu wakiiona kuwa inameza haki zao na kuwaburuza kidikteta lakini walikuwa wakiielekea na kujaribu kuirekebisha mioyo na akili zao, kwa sababu ilikuwa serikali yao kwa hali zote. Hao (Waislamu) walikuwa na upungufu katika kufahamu hakika ya mwamko na kufahamu twariqa yake katika kuirekebisha hiyo serikali yao, na haukupatikana kati yao muundo wa chama sahihi, na tunaweza kuhukumu kwamba wengi ya Waislamu walikua hivi.

Lakini katika wakati huo huo tayari ilikuwa thaqafa ya kigeni imevamia biladi za Kiislamu na kwa kupitia thaqafa hiyo wakoloni wakaweza kuwavutia baadhi ya Waislamu (kijikundi cha Waislamu) waliowachochea kusimamisha vikundi vya kichama ndani ya serikali ya Kiislamu vilivyo simama juu ya msingi wa kujitenga na kudai uhuru. Na wakoloni wakaweza kwa sura maalum kuwavutia baadhi ya waarabu walio wakusanya Paris ili kutengeneza kwa kupitia wao kikundi kitakachopiga vita serikali ya Kiislamu ya Uthmaniya kwa jina la uhuru wa waarabu. Thaqafa hiyo ya kigeni ndio iliyowakusanya pamoja na fikra za kikoloni na hisia za kizalendo na ukabila zilizopandikizwa na kafiri mkoloni ndani yao, mpaka ikawa fungamano lao la kiakili na kihisia ni moja na mantiki moja iliyowakusanya hadi kuwafikisha kuunganisha lengo, nalo ni uhuru wa taifa la kiarabu eti kwa sababu serikali ya Uthmaniya imedharau maslahi yao na ikajihalalishia kuwadhulumu na kula haki zao. Likawa lengo hilo la jumuiya ni mbinu ya kuunda juu yake kikundi cha chama kijina kilichofanikisha kwa kuandaa vuguvugu lililoitwa la kiarabu na kuzaa natija ya kueneza udhibiti wa makafiri na ukoloni juu ya biladi za Kiislamu na hususan biladi za kiarabu. Kazi za vyama hivi ikamalizikia hapa na wakagawanyiwa ngawira kwa kupewa kwao hatamu za kuwa viongozi wa baadhi ya biladi za Kiislamu kama vibaraka wa ukoloni huu.

Baada ya kuondoshwa serikali ya Kiislamu katika nyanja za kimaisha, ukoloni ukachukuwa nafasi yake na kutawala biladi za kiarabu moja kwa moja na kueneza udhibiti wake kulikobakia katika biladi za Kiislamu. Walivamia biladi za kiarabu moja kwa moja na wakaanza kutawalisha na kukita nguvu zao bara bara sehemu zote kwa mbinu na njia zao chafu na za siri, thaqafa ya kikoloni ndiyo iliyokuwa mbinu kuu, hongo ya pesa na kuwaweka Vibaraka.

Thaqafa ya kikoloni ilikuwa na athari kubwa katika kumakinisha ukafiri na ukoloni, na katika kuzuiya mwamko sahihi, na kusambaratika kila harakati imma ziwe za kijumuia au za kichama, kwa sababu thaqafa ina athari kubwa juu ya fikra ya binadamu na inaathiri mwenendo (muelekeo) maishani. Ukoloni uliweka manhaj ya masomo na thaqafa (elimu ya kurithi ya kiitikadi au mila) juu ya msingi wa falsafa thabiti nayo ni mtazamo wa kimagharibi katika maisha, ambao ni kutenganisha mada na roho na kutenganisha dini na serikali. Na ukoloni ukafanya shakhsiyya (utambulisho) yake ndio chimbuko la thaqafa yetu. Na ukafanya hadhara (ustaarabu) yake na fikra zake na misingi ya nchi yake na historia yake na mazingira yake ndio chimbuko msingi la mambo tunayojaziwa akilini mwetu. Wala haukutosheka na hayo, bali pia ukafanya mkorogo wa makusudi wa sisi kutunywesha shakhsiyya yake, fikra zake na fahamu zake. Na ikaficha sura halisi ya ukoloni kwa kuipigia debe shakhsiyya yake na kuipa daraja la juu la kustahiki kuigwa na hadhi madhubuti ambayo hakuna maendeleo pasina kuwa nayo, huku ikificha sura halisi ya ukoloni kwa mbinu chafu. Kisha ukoloni ukaingilia katika upangaji wa mitaala (*barnamij*) mpaka hata mambo madogo madogo yasende kinyume na mitaala mama wa masomo. Kwa hivyo tukawa tunasomeshwa thaqafa chafu inayotufundisha vipi wengine wanavyofikiri, na kimaumbile tushindwe namna ya kufikiri. Kwa sababu fikra yetu ipo mbali na mazingira

yetu na shaksiyya yetu na historia na pia haikuegemea mfumo wetu. Hivyo tukawa sisi wenye kuitwa wasomi tupo mbali na Ummah wetu, tusiofahamu mazingara yetu wala shida za Ummah. Kwa hivyo, zikawa hisia za wasomi zimetengana na fikra na akili zao na wakawa wasomi kimaumbile wako kando na hisia za Ummah na machungu ya Ummah. Na ikawa kimaumbile fikra haiwezi kuleta ufahamu sahihi juu ya hali ilivyo wala haileti ufahamu sahihi wa kujuwa hali ya Ummah. Na wala haileti ufahamu wa kindani ya njia ya mwamko. Kwani ilikuwa ni fikra iliyotengana na hisia zake. Kama sikuwa tupu na hisia. Licha ya yote hayo ilikua ni fikra ya kikoloni iliyyobebwa na mtu mwenye hisia za Kiislamu. Fikra hii ikawa kimaumbile haiwezi kuleta kikundi sahihi kilichopata ufahamu sahihi. Na athari ya thaqafa ya kikoloni haikuishia kwa wasomi peke yao bali ikawa fikra ya mujtama mzima kutokana na msukumo wa kififikra ambazo zimo ndani ya fikra zilizo kando na hisia zake. Na kwa sababu hii tatizo likawa sugu zaidi katika mujtama na mzigo ukaongezeka kwa kikundi sahihi kuliko ilivyokuwa hapo kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Kwani tatizo lililokuwa likiukabili Ummah au kikundi sahihi cha kichama ni kuleta mwamko tu katika mujtama wa Kiislamu. Lakini tatizo limekuwa ni kuoanisha baina ya fikra na hisia kwa wasomi. Na kuoanisha baina ya mtu binafsi na jamii yake katika fikra na hizia hasa hasa baina ya wasomi na mujtama wao. Kwa sababu hawa wasomi walikuwa wamejitolea kikweli kutetea fikra ngeni, zisizokuwa na hisia, na kujitolea huku kukawapelekea kuudharau Ummah na kujitenga nao na kutoujali kama ilivyowapeleka kuwapenda wakoloni na kujipendekeza na kuwapa umuhimu japo kuwa ni wakoloni. Na kwa hivyo haiwezekani kwa msomi kama huyu kufikiria hali halisi (ya matatizo) iliyo katika biladi yake isipokua kwa kumwigiza mkoloni namna ya kufikiri katika mji wake (mkoloni) pasina kufahamu hakika ya dhurufu hizi. Basi akawa hajui kitakacholeta mwamko kwa Ummah ila kwa kumwigiza mkoloni pindi anapozungumzia juu ya miamko. Wala hisia za msomi huyu hazijiingizi katika vuguvugu la mabadiliko (kuhamasika) kwa ajili ya mfumo bali hisia zake huingia katika vuguvugu kwa ajili ya uzalendo na watu. Na huu ni mchangamko wa kimakosa. Pamoja na hayo, hajitosi (msomi) katika vuguvugu la kweli linapopamba moto kwa ajili ya mji wake wala hajitoi muhanga kikweli kwa ajili ya watu wake, kwani yeye hahisi hisia za kififikra juu ya dhurufu zilizomzunguka wala hahisi hisia za kififikra juu matatizo ya watu. Hata tukisema (tukijaalia) kuwa alisimama kwa lengo la mapinduzi na kutafuta mwamko, huwa ni msimamo uliotokana na mgongano wa maslahi yake binafsi tu (ikiwa ameguswa katika maslahi yake) au ni msimamo wa kukurupuka kwa kudandia vuguvugu la watu. Kwa hivyo haitochukuwa muda kupotea pindi utakapomalizika mgongano kwa kumpa cheo au kuridhisha tamaa zake au hupotea pindi itakopo gongana na maslahi yake binafsi na manufaa yake au anapokutana na matatizo.

Na mfano wa msomi kama huyu, haliwezi kupatikana kundi sahihi kutoka kwake isipokuwa baada ya kumtibu upya kwa kuzioanisha fikra zake na hisia zake na thaqafa kwa kumsomesha upya thaqafa ya kimfumo iliyo sahihi, yaani thaqafa ya Kiislamu. Na tiba yake italazimisha awe mwanafunzi, utengenezwe upya ufahamu wake mpaka baada ya kutatua tatizo hili aingie hatua inayofuata ya kuunganisha kati ya fikra zake na hisia zake na kati yake yeye na jamii yake hapo ndipo itakuwa rahisi kutatua tatizo la mwamko katika mujtama. Na lau kama si thaqafa ya kikoloni basi kurudisha mwamko ingelikuwa jambo rahisi sana kuliko hali ilivyo leo.

Hivyo basi haiwezekani kwa thaqafa hii ya kikoloni iliyopo katika mujtama ilete kikundi kilicho sahihi cha kichama, au kupatikane chama sahihi juu ya msingi wa thaqafa ya kimagharibi. Na ukoloni haukutosheka na thaqafa yake tu bali ukavuruga na kuharibu anga kwa kupandikiza fikra, rai za kisiasa, za falsafa zilizo haribu mtizamo wa maisha wa sawa kwa Waislamu. Na ukavuruga kwa kuharibu anga safi la Kiislamu na kukoroga fikra kwa Waislamu mkorogo wa wazi katika kila nyanja ya maisha. Hivyo basi ukoloni ukawakosesha Waislamu jambo msingi la kimaumbile linalowapa uhai wa Uislamu wao. Na mkoloni akazivuruga harakati zote zenye kutaka kuleta mwamko, tahamaki zikawa zenye

kuchanganyikiwa na zenye mgongano zinazofanana na mwenye kutupatupa miguu anaechinjwa, zinaishia kwenye kupigwa na butwaa na kukata tamaa na kusalimu amri. Kwani mkoloni alifanikiwa kutumia fursa kwa kufanya shakhsiyya yake ndiyo kituo kikuu cha mzunguko mzima wa thaqafa na ndio kimbilio la wanasiasa na akafanya ndio kibla cha mtazamo wa wanasiasa na wasakatonge wa kisiasa kwa kutaka msaada kwa mkoloni na kumtegemea. Basi harakati nyingi zikawa pasi na kujitambua zikitaka msaada kwa mkoloni. Wakapatikana watu katika nchi walioona kuwa kuchukuwa msaada kwa mkoloni inafaa bila ya kujua kuwa usaidizi wowote wa mkoloni na kupigia debe kumtegemea mkoloni wa aina yeyote ni kunywa sumu ya mkoloni na ni khiyana kwa Ummah hata kama ni kwa nia nzuri. Na wakawa hawajui kuwa kufungamanisha maswala yetu nyeti na wasiokua sisi ni kujinyonga kisiasa. Hivyo, haiwezekani kupatikana mafanikio kwa kusimama harakati yoyote iliyomeza sumu ya mkoloni ya kumtegemea au kumpigia debe.

Na pia ukoloni ukaupa sumu mujtamaa kwa uzalendo na ukaumia na ujamaa kama vile ulivyotia sumu fikra ya kupenda kujitenga ukafanya fikra ya ubinafsi ndio kichocheo cha kudai mwamko. Na kama ulivyotia sumu ya kutowezekana kusimama tena dola ya Kiislamu na kutowezekana kupatikana umoja katika miji ya Kiislamu eti kwa kuwepo tofauti ya kimiji, kitabaka na lugha japokuwa Ummah wote ni Ummah mmoja, na hali ya kuwa aqida ya Kiislamu ina wakusanya pamoja, aqida ambayo inazaa nidhamu za maisha. Na pia wakaumezesha Ummah fikra nyingine za mitazamo ya kisiasa iliyokorogeka mfano **“chukuwa (kilichopo) kisha endelea kuomba”** au **“Ummah ndio chimbuko la utawala”** pia **“mamlaka (ubwana) ni kwa raia”** na mengineyo**.** Na ukautia sumu Ummah kwa kuujaza fikra potofu mfano matamshi yao ***"Dini ni ya Mwenyezi Mungu na nchi ni yetu sote (kutenganisha serikali na dini)”***, au ***“tunaungana katika matatizo na matarajio (hatuunganishwi kwa fahamu)’*** **pia** ***“nchi ipo juu ya kila kitu” na “utukufu ni wa nchi”*****,** na yanayo fanana na hayo. Na pia Ummah ukatiwa sumu na fikra za kutaka kufuata hali halisi **(pragmatism) (badala ya Uislamu).** Kwa mfano: ***“hakika sisi tuna chukua taratibu zetu za maisha kutoka kwenye hali halisi tuliyonayo”*** au lazima kukubaliana na hali halisi na ***“au ni lazima tuwe watu wa hali halisi”*****,** na yanayo fanana na haya.

Na kutokana na athari ya sumu hizi ikawa katika mujtama wa Kiislamu zikiwemo biladi za kiarabu zikawa katika hali ambayo haiwezekani kupatikana kikundi sahihi. Hivyo haikuwa ajabu kuporomoka harakati zote za kichama kijina kwani hazikusimama juu ya msingi wa fikra madhubuti inayopangilia mambo kimakini na kupanga mikakati yenye kuaminika. Bali zilisimama kinyume na msingi huu. Na mpaka hapa ilikuwa ni jambo la kimaumbile kwa harakati zilizosimama katika ulimwengu wa Kiislamu na hasa wa kiarabu ziwe ni harakati zenye kusambaratika kwani zilisimama juu ya msingi usio kuwa wa kimfumo.

Na mwenye kuzichunguza harakati hizo kwa umakini ataona kuwa zilisimama juu ya kuzuka kwa matukio yaliyo sababishwa na hali fulani ndio yakasababisha kuzuka kwa vikundi hivyo na mara tu yalipo malizika matukio hayo na harakati hizi nazo zikapotea au zikazorota na kudidimia. Au harakati hizo zilisimama juu ya msingi wa urafiki baina yao , na urafiki huu ukawaunganisha na wakaanzisha kikundi kwa msingi huu, na kundi hili likaishia kwao wao wenyewe tu. Au juu ya msingi wa maslahi ya kibinafsi au yasiyokuwa hayo. Hivyo, halikuwepo baina ya watu walio jikusanya juu ya misingi huu katika mazingira haya na mujtama huu, fungamano la kichama la kimfumo, basi kupatikana kwake (vikundi hivi) si tu kutokuwa na faida bali ikawa ni madhara kwa Ummah, na zaidi ya hayo kuwepo kwake ndani ya mujtama vinazuyia kupatikana kikundi cha kichama kilicho sahihi au vinachelewesha kujulikana (na jamii) kwani vinapandikiza hali ya kukata tamaa kwa watu na vinaharibu nyoyo, kutia weusi na wasiwasi na vinasababisha harakati yoyote ya kichama itiliwe mashaka hata kama ni sahihi (na imepatia njia). Na zinapandikiza kwa watu chuki binafsi na chuki za kiukoo na zinawafunza watu kwa mbinu zake kutapatapa nyuma ya maslahi na kwa lugha nyingine zinaharibu tabia nzuri ya jamii na zinazidisha

mzigo kwa vikundi vya kichama vitakavyokuwa sahihi vitakavyochomoza, na ni lazima vichomoze kutoka ndani ya Ummah.

Na sambamba na harakati za Kiislamu na za kikabila na za kizalendo zikapatikana harakati za kikomunisti. Hizi zilisimama juu ya msingi wa kimada (kutoamini Uungu), harakati hizi zilikuwa zinafuata harakati ya kikomonisti ya Urusi na zikichukuwa maelekezo yake kutoka kwa mrusi. Na njia yao "ya kufikia malengo" ni bomoa bomoa na uharibifu. Na malengo yake makuu japo ni kueneza ukomunisti katika nchi za Kiislamu ni kuvuruga ukoloni wa kimagharibi kwa maslahi ya kambi ya mashariki. Walikuwa wanaharakati wa kikomunisti wakiwashutumu wanaharakati (watawala, wanaharakati wa kitaifa na wanaharakati wa Kiislamu) kuwa ni vibaraka wa magharibi lakini Ummah haukuziitikia harakati hizi, na wala hazikuleta athari. Na kupotea kwake ilikuwa ni suala la kutarajiwa kwani zinapingana na umbile (fitra) ya mwanaadamu na zinagongana na itikadi ya Kiislamu hii ni kutokana na madai yao kuwa hakuna Mwenyezi Mungu. Harakati za kikomunisti zilitumia uzalendo kwa malengo yake na likawa ni tatizo juu ya matatizo ambayo mujtama unateseka nayo.

Na zilikuwa baadhi ya harakati juu ya msingi wa muungano, zikachipuza ndani ya nchi mashirika ya kimaeneo na ya kimajimbo yanayokusudia kufanya mambo ya kheri, zikaasisi mashule na hospitali na makambi ya wakimbizi, na zikasaidia katika mambo ya khairat, na uozo wa uzalendo ulikuwa umezighubika harakati hizi, na ukoloni ulizisaidia mpaka shughuli za jumuiya hizo zikaonekana wazi wazi kwa watu kwamba zinaweza kusaidia. Na nyingi zilikuwa ni taasisi za kielimu na misaada na hazikupatikana taasisi za kisiasa ila chache sana.

Na ikichunguzwa kwa jicho la umakini faida za taasisi hizi itaonekana kuwa hazikuleta faida yoyote inayonufaisha Ummah au kusaidia kuleta mwamko, na madhara yake ni yaliyo fichika kiasi hayawezi kuonekana ila kwa mchambuzi hodari, kwa kuwa ile kuwepo kwake tu jumuiya hizi ni madhara makubwa bila kuangalia manufaa kidogo (kwa mtu mmoja mmoja). Nayo ni kwamba Ummah wa Kiislamu kwa ujumla wake na kwa kuwepo baadhi ya fikra za Kiislamu na kutekeleza baadhi ya hukmu za Kiislamu na kwa kuwepo baadhi ya hisia za Kiislamu kwa athari ya Uislamu zinapatikana hisia (ihsaas) za kutaka mwamko na kuna hisia za kusaidiana kimaumbile (aatwifatu) na kuna msukumo wa kimaumbile wa kuanzisha kundi kwani roho ya Uislamu ni roho ya kipamoja (mjumuiko). Lau Ummha wa Kiislamu utawachiwa pasina kushugulishwa na mengine hisia hizi hugeuka kimaumbile kimantiq na kuwa fikra, na fikra hii itazalisha kazi ya kuleta mwamko wa Ummah. Lakini kwa kupatikana jumuiya hizo (za misaada) zilizuiya kupatikana hali hiyo kwani zilikuwa zinatoa joto lenye mihemko (ndani kwa ndani) na kulipeleka hisia kwenye vijikazi hivi, nayo ni mtu kupewa uanachama kwenye taasisi hizi, basi mwanachama wa taasisi hizi atajiona amejenga madrasaau ameanzishahospitali au ame changia katika kazi za kheri, hapo anahisi raha na utulivu na ana jifakhari kwa kazi hii. Hali hii ingekua tofauti lau kama zisinge asisiwa taasisi hizi, hakika ile roho ya pamoja itamsukuma kujiunga na kikundi sahihi ambacho ni kikundi cha kichama kitakacholeta mwamko sahihi.

Na sambamba na taasisi hizi za kielimu na khairat zikasimama taasisi za kulingania akhlaqi zinazofanya kazi kwa lengo la kuinua Ummah kwa kupitia akhlaaq. Kwa kutoa mawaidha na nasaha na mihadhara na matoleo kwa mazingatio kuwa akhlaqi ndio msingi wa mwamko, na harakati hizi zimetumia juhudi kubwa lakini hazikuwa na faida yoyote kubwa. Nazo pia zikatoa joto la Ummah kwa mazungumzo au mada za kuchokesha na kurudiwarudiwa. Na usimamaji wa harakati hizi ulijengeka juu ya ufahamu wa kimakosa juu ya kauli ya Mwenyezi Mungu akimukhutubia Mtume (saw) ***"Na hakika wewe una tabia nzuri***." [TMQ Al-Qalam: 4] Licha ya kuwa kiudhati aya hii inamsifia Mtume (saw) kama Mtume na sio kusifiwa mujtama mzima. Na juu ya kauli ya Mtume (saw): ***"Hakika***

***Mwenyezi Mungu Amenituma mimi kwa lengo la kutimiza akhlaq nzuri”***, na pia juu ya kauli ya (saw) “***hakika nimetumwa ili kukamilisha akhlaqi nzuri”*** japo hadithi hizi mbili na mfano wake ni hadithi zinazo zungumza juu ya sifa ya mtu binafsi na si juu ya mujtama.

Na pia (harakati za kiakhlaq) zilijengwa juu ya ufahamu wa kimakosa wa mshairi aliposema, ***"hakika si vyengine, hadhi ya Ummah ni watakaposhikana na akhlaqi, ikiwa akhlaqi zao zitaondoka basi na wao wataondoka (poromoka)."*** Japokuwa Ummah haunyanyuki kwa akhlaqi bali unanyanyuka kwa aqida ambayo wameiamini na fikra zinazobebwa na Ummah na nidhamu wanazo zitawalisha. Na hili pia lilikuwa limejengewa juu ya ufahamu wa kimakosa wa maana ya mujtama eti kuwa mujtama unajengeka juu ya mtu mmoja mmoja japo ya kuwa mujtama unajengeka juu ya vitu vinne: mwanadamu, fikra, hisia na nidhamu. Na kuharibika kwake inakuwa ni kwa kuharibika fikra, hisia na nidhamu na si kwa kuharibika mtu mmoja, na marekebisho yake yanakuwa kwa kurekebisha fikra, hisia na nidhamu zake.

Na makosa haya yalitokana kujengeka ufahamu kwa wenye kudai kurekebisha jamii (muslihuna) na wanaojiita wataalamu wa akhlaq, kwamba mtu binafsi ndiye anaye haribu jamii na yeye anaharibiwa na tabia (akhlaqi) au kutengenezwa na tabia (akhlaqi), hivyo basi tabia nzuri humfanya mwenye nazo kuwa mtu bora, mwenye msimamo, bidii na faida, mchapakazi katika mambo ya kheri, mwema na mwenye kulingania. Na tabia mbaya zinamfanya kuwa dhaifu, mzembe, asiye na manufaa, hana kheri yoyote, hana katika maisha haya isipokuwa kushibisha matamanio yake na ubinafsi wake. Hivyo basi wakaona kuirekebisha jamii ni kupitia kumrekebisha mtu binafsi, wakataka kuurekebisha mujtamaa kwa kutumia njia ya akhlaqi na watumie akhlaqi kuleta mwamko wa Ummah.

Licha ya kufeli kwa harakati zote zilizosimama juu ya msingi wa akhlaqi, ila bado kuna watu wanaamini kuwa msingi huo wa kiakhlaqi bado ni msingi wa mabadiliko, na wakaanzisha jumuiya za kutaka mabadililiko juu ya msingi huu. Japo hakika ya mambo njia ya kuirekebisha jamii si njia ya kumrekebisha mtu binafsi hata kama na yeye ni sehemu katika jamii, kwani kuharibika kwa jamii kunatokana na kuharibika hisia zao za kijumla (jamii) na kuharibika mazingira yake ya kififkra na kiroho, na pia hutokana na kuwepo fikra mkorogeko kwa jamii. Au kwa maneno mengine hutokana na kuharibika tabia jumla *(urfu aam)* na marekebisho yake hayaji ila kwa kuleta tabia jumla nzuri *(urfu aam)* yaani haiwi ila kwa kurekebisha hisia za jamii na kuleta mazingira ya kiroho yaliyo safi na kuleta mazingira ya kifikra ambayo yataungana na upande wa kiroho na kwa upande wa serikali ni kutawalisha nidhamu. Na hilo halitowezekana isipokuwa kwa kuleta mazingira ya Kiislamu na lazima kurekebisha fahamu za watu wote juu ya vitu. Kwa kufanya hivi jamii itarekebishika na mtu binafsi pia atarekebishika. Na hilo haliwi kwa kupitia vyama vilivyo juu ya msingi wa kijumuiya wala kwa kufanya akhlaqi, mawaidha na elimu kuwa ndio msingi wa kuunda kundi hilo.

Mpaka hapa imekuwa kudorora kwa harakati hizi zilizo juu ya msingi wa kijumuiya katika kuleta mabadiliko na mwamko kama zilivyodorora harakati zote zilizoundwa juu ya msingi wa chama kijina ambazo hazikujengewa juu ya mfumo maalumu na hazikuwa na ufahamu wowote na hazikufanya fungamano lake juu ya msingi thabiti wenye kuwajumuisha watu. Pia kudorora kwa harakati hizi zote lilikuwa ni jambo la lazima kutokana na wanachama wake, kwani licha ya kwamba ziliundwa juu ya msingi mbovu kwa kutokuwa na fikra na twariqa na kukosea njia katika uundaji wa chama, kwani zilikuwa hazina kipimo maalum kwa mujibu wa harakati kufaa kwa mwanachama bali zilikuwa zinampima mtu kwa mujibu wa nafasi yake katika mujtama na uwezekano wa kuleta manufaa ya haraka kwa kuwepo kwake katika chama au jumuiya.

Mwanachama alikuwa ana chaguliwa kwa kuwa yeye ana hadhi katika jamii yake ima tajiri, wakili, au daktari au kauli yake ni yenye kusikilizwa katika jamii, pasi na kuangalia kufaa kwake au kutofaa kwake katika chama hicho kinacho mchagua. Hivyo basi vyama hivyo vilikuwa haviishi kugawika baina ya wanachama wake, kama vile ambavyo utabaka ulikuwa ukiwatokea. Wanachama wa jumuiya walikuwa wakijihisi kindani kuwa wao ni bora kuliko watu wengine si kwa mali zao na vyeo vyao tu bali kwa kuwa kwao ni wanachama wa chama au taasisi fulani. Hivyo walikuwa hawana uhusiano mzuri wala ukaribu na watu. Ikawa kupatikana kwa jumuiya hizi na vyama hivi ni balaa juu ya balaa na ni tatizo jipya lenye kuongeza matatizo ambayo mujtamaa una hangaika nayo.

Hivyo tunaweza kusema baada ya kusoma, kufikiri na kuchunguza biladi za Kiislamu zote katika karne iliyopita halikupatikana kundi sahihi lenye uwezo wa kuleta mwamko. Na harakati zote zilizopatikana ziliporomoka kwani zilisimama juu ya msingi uliokorogeka, licha ya kwamba Ummah hauwezi kunyanyuka ila kwa kupitia kikundi, basi ni kikundi gani sahihi ambacho kitaleta mwamko wa Ummah. Haya ndio ambayo tunataka tufafanue:

Hakika kundi sahihi ambalo linaweza kunyanyua Ummah halifai liwe juu ya msingi wa kijumuiya ambao msingi wake una lazimisha uwe juu ya vitendo na maneno au vitendo tu au maneno tu, na aina hii ya kikundi haifai kishajiishwe katika Ummah ambao unataka mwamko na wala haijuzu kiwe juu ya msingi wa vyama visivyokuwa vya kimfumo, kama vile ambavyo vilisimama katika ulimwengu wa Kiislamu tokea Vita ya Kwanza mpaka leo.

Hakika kundi sahihi ni kundi ambalo linasimama juu ya msingi wa chama cha kimfumo wa Kiislamu, na iwe fikra ndio roho ya mwili wa chama na ndio kiini chake na ndio siri ya uhai wake, na itakuwa mbegu ya mwanzo ni mwanadamu ambaye zitamwingia fikra na njia yenye kutokamana na fikra hiyo mpaka awe mwanadamu huyo yeye ndio fikra (na fikra ndio yeye), katika kung'ara kwake na usafi wake, na awe mfano wa kuigwa katika njia na msimamo wake. Pindi kutakapo patikana vitu hivi vitatu, fikra iliyokomaa, njia iliyo wazi na mtu msafi. Basi mbegu ya kwanza itakuwa imepatikana, kisha haitachukua muda mbegu hii itaongezeka zitakuwa mbegu nyingi na wao ndio halaqah ya kwanza na kutakapo patikana halaqah ya mwanzo basi kundi la kichama litakuwa limeanza kuchipua. Kwani halaqah hii haitachukua muda litakuwa ni kundi, na kundi hili litahitaji fungamano la kichama litakalo wakusanya watu ambao wameamini fikra na njia. Fungamano hili la kichama ni aqida ambayo mtazamo wa chama utatoka ndani ya aqidah hiyo na thaqafah ambayo chama kitajipamba na fikra zake, muda huo itakuwa kikundi cha kichama kimesha jitengeneza na kitaweza kuingia katika maisha, kitakutana na hali za joto na baridi, kitapitiwa na upepo mzuri na mbaya na mabadiliko ya mazingira mepesi na magumu, kikiweza kuthibiti katika vikwazo hivyo, kimeshasafika kifikra, na njia yake itakuwa imeshakuwa wazi na kitakuwa kiliwaandaa vizuri watu wake na fungamano lake lilikuwa madhubuti, na ndio kikaweza kupiga hatua ya kivitendo na kufanya kazi kutoka katika kundi la kichama mpaka kuwa chama cha kimfumo kilicho kamilika, chenye kufanya kazi kuleta mwamko ulio sahihi. Hilo ndio kundi sahihi ambalo kiini chake ni fikra, kwani fikra ndio mzizi wa uhai.

Ama vipi huanzishwa kimaumbile kundi hilo la kichama la kimfumo katika Ummah unaotaka mwamko, ufuatao ni ufafanuzi wake:

Ummah ni mwili mmoja haugawiki vipande, na katika umbile lake ni kama mwanadamu hupatwa na maradhi mazito akakaribia kufa, kisha akaanza kupata nafuu, hakika ya nafuu hiyo huenea mwili mzima, basi ndivyo ulivyo Ummah ulioporomoka huchukuliwa kama mgonjwa, uhai ukianza kuenea katika Ummah utaenea mwili mzima kwa sifa yake kama ni mtu wenye kuzingatiwa kuwa ni kitu kimoja, na uhai wa Ummah ni fikra yenye kwenda sambamba na njia yenye kutokamana na fikra hiyo hiyo, na waitekeleze. Na mkusanyiko huo (wa fikra na twariqa) ndio huitwa mfumo.

Na si tu kupatikana mfumo inatosheleza kuleta mwamko, bali mfumo uwe wa kweli na uwekwe katika utekelezwaji maishan. Hilo ndilo jambo litakalofanya Ummah uwe hai, kwani Ummah unaweza kuwa na mfumo katika urithi wake wa kisheria, kithaqafah na kitareekh lakini wakawa wameghafilika nao, au wameghafilika na fikra ya mfumo huo au wameghafilika na njia au wameghafilika kuviunganisha (baina ya fikra na njia). Katika hali kama hii kuwepo tu kwa fikra na twariqa hakutoshelezi kuleta mabadiliko.

Na kawaida uhai huenea kwa Ummah panapokuwa na matatizo mazito katika mujitama ambayo husababisha kupatikana hisia za kipamoja, na hisia hizi za mjumuiko zitaleta kufikiria mambo nyeti kutokana na kuchambua chanzo cha kuzalika kwa matatizo hayo na mbinu za karibu na za mbali za kujinasua.

Isipokuwa hisia hizi hata kama zitaungana zikawa ni hisia moja katika kundi hazitakuwa daraja moja kwa wanakundi na hii ni kwa mujibu wa mtu alivyo ruzukiwa na Mwenyezi Mungu, walivyopewa uwezo wao wa vipawa, hivyo basi uongofu wa fikra utakuwa umo ndani yao mpaka athari yake itakapo jikusanya, itachipuka na kukita katika hao ambao walio ruzukiwa uwezo wa juu wa hisia, watawamsha wenzao na watawazindua na watawaenezea uhai. Hivyo basi uhai wa Ummah utaanzia kwa watu hawa.

Hawa walio pewa uwezo wajuu ya hisia kimaumbile wanazo hisia za ulazima wa kuwepo kundi na fikra itakita ndani yao basi wataanza kufanya harakati kwa ufahamu welezi na ukomavu na wao ndio jicho la Ummah na ndio kikundi chenye ufahamu makini. Lakini mwanzoni kundi hili lenye ufahamu litakuwa limeshikwa na butwaa likiona hali tofauti tofauti na kutahayari njia ipi lishike. Kiwango cha utambuzi ndani ya kundi hilo itatofautiana miongoni mwa wanachama wake. Itakuwa mantiki ya hisia iko juu kuliko wengine, basi kutapatikana kutoka ndani ya kundi hili lenye ufahamu watu wenye ufahamu bora zaidi, watachagua mwelekeo maalum baada ya kuisoma hali halisi ilivyo wataona lengo lao ambalo wanataka walifikie kama vile ambavyo wataona njia yao na kuelekea lengo hilo. Hivyo basi, watauelekea mfumo kwa fikra na twariqa na wataiamini hali ya kuwa ni aqida iliyokita na wata vaana nao mpaka uwe (mfumo) ndio aqida yao. Aqida hii pamoja na thaqafah ya chama ndio itakuwa fungamano la wanachama wake.

Na mfumo utakapovaana na watu hawa hautoweza kufichika, bali utawasukuma watu hawa kwa ghera kubeba da'wah, kazi zao zitapangiwa na mfumo, zitakwenda kwa mujibu wa manhaji ya mfumo, zitafuata miiko iliyowekwa na mfumo, kuwepo kwao ni kwa ajili ya mfumo na kwajili ya da'wa na kubeba majukumu ya mfumo na da'wah hii inalenga kuwakinaisha watu wauamini mfumo huu pekee na kuleta ufahamu jumla **(**WAI AAM**).** Hivyo halaqa hii itageuka kuwa kikundi, kisha kuwa chama cha kimfumo, kitaanza kukua kimaumbile katika mambo mawili; kuongezeka kwa kuleta viini vingine vitakavyo amini mfumo na kuufahamu vizuri na kuleta WAI AMM (ufahamu jumla) kwa ummah mzima. Ummah utaungana kijumla (ufahamu ambao haujamakinika) au utaungana kwa pamoja (ufahamu uliomakinika). Hivyo basi lengo la Ummah litakuwa moja, nalo ni aqida yake moja namtazamo wake mmoja. Hivyo chama kitakuwa ni mtambo wenye kuyeyusha Ummah. Utausafisha kutokana na uchafu na ufisadi ambao ulisababisha Ummah kuporomoka au uliozaliwa katika zama za mporomoko. Chama ndio kitasimamia mchakato huu wa usafishaji ndani ya Ummah, mpaka pale Ummah utakapo kuwa na mwamko. Hii ni kazi nzito ambayo haitawezwa isipokuwa na chama ambacho kinaishi kwa mujibu wa fikra zake, imejifunga na fikra zake ndani ya maisha jumla na ina fahamu kila hatua inayopiga.

Ni hisia ambazo zitapelekea kuunda fikra ya chama hiki. Fikra hii itang'ara katika Ummah miongoni mwa fikra nyingi. Mwanzo wake itakuwa dhaifu kwa sababu ni changa zaidi kuzaliwa na kuanzishwa na bado haijamakinika na wala haijapata maeneo. Lakini kwa sababu fikra hii ni matokeo ya mantiki ya hisia, yaani ufahamu uliotokana na ufahamu wa kihisia, kwa hakika yake huleta hisia za kifikra. Hivyo basi, huleta hisia za wazi kwani ni matokeo ya fikra za kina basi inakuwa – kwa maumbile yake humsafisha yule anayo ambatana nayo, na humfanya awe ni mwenye ikhlasi, hata kama akitaka asiwe ni mwenye Ikhlasi hawezi kufanya hivyo, na inakuwa fikra hii ndio Itikadi na thaqafa kwa mwenye ikhlasi. Hivyo basi, itamletea mapinduzi katika nafsi yake mapinduzi makubwa. Na haya mapinduzi si chochote zaidi ya kuwa ni mrimpuko baada ya kuungua katika hisia na fikra. Na huchochea katika da’wah ghera, hamasa na ukweli, kama vile huchochea mantiki na fikra na anakuwa ni moto unaounguza ufisadi, na nuru inayo angaza njia ya mafanikio, kwa sababu hii huwa da’wah ipo katika mapambano dhidi ya fikra chafu, na itikadi mbovu, na ada au tabia chafu, na zinajaribu kujihami zenyewe . Lakini kule kujihami kwake kunakuwa kwa msuguano na mfumo mpya, huzidisha nguvu zake. Na mpambano huu utaendelea mpaka fikra, itikadi na njia zote kombo zitatoweka na utabakia mfumo wa chama pekee katika Ummah utakuwa ndio mfumo wake na aqida yake.

Na muda wote chama kitakapoweza kuziunganisha fikra zote na itikadi na rai kuwa moja, kitakuwa kimetengeneza umoja wa Ummah kwa umakini na uhodari, kuusafisha,na kuutakasa Ummah basi hapo Ummah utakuwa ni mmoja na utapatikana umoja wa kikweli. Kisha inakuja hatua ya pili ya chama, nayo ni kuuongoza Ummah kufanya kazi ya mabadiliko ya kimsingi na kimapinduzi, ili kuunyanyua ummah, kisha kibebe pamoja nao ujumbe wa Uislamu kwa wengine katika watu (Ummah mbali mbali), ili iweze kutekeleza wajibu wake wa kibinadamu.

Muundo huu wa chama ndio harakati ya kikundi, na wala haiwezekani isipokuwa lazima iwe ni harakati ya kikundi, kwa sababu muundo sahihi hauwezi kuwa ni harakati ya mtu mmoja mmoja. Kwa sababu hii imekuwa ni lazima kwa wasimamizi wa chama katika miji ya Kiislamu wafanye utafiti wa kina katika harakati za makundi, na wazifahamu ufahamu wa kina.

Na kufahamu harakati za makundi ambazo zina nguvu za kuathiri katika wakati wake, kunatuonyesha kuwa hazianzishwi wakati kuna raha na wepesi, na haki za kimaumbile za mwanadamu zinapatikana kwa uhakika, na maisha mazuri yapo na wakati inapokuwa kustahiki kwa mtu binafsi ndio kipimo cha kusimamia mambo muhimu.

Na kufahamu harakati hizi za makundi unatufanyia wepesi kuzipima harakati zote za kimakundi kwa kipimo chake cha sawa sawa. Kwa kusoma mazingira ambayo imewahi kuwa nayo au iliyo nayo sasa hivi. Na mazingira ambayo ilikumbana nayo au inakumbana nayo na kujua juhudi za wafuasi wake mahodari na athari zao katika kuendesha harakati hiyo na kuirahisishia harakati hiyo vikwazo ambavyo vina ikwamisha katika kufaulu au kupiga hatua.

Na hupimwa uwezo wa harakati kufaulu kwake uwezo wake wa kuamsha hisia za watu na kuwashawishi kupinga dhulma kila mamlaka itakapo zidisha dhulma au mfumo uliopo hasa katika mambo yanayogusa mfumo wake huu (Uislamu) au serikali kupelekwa kwa matamanio.

Na kufahamu harakati hizi za kivikundi ina tulazimu kuyasoma maisha ya mujtama na kujua mahusiano yapo vipi baina ya Ummah na serikali na vipi watawala wapo na Ummah na misingi ya kila mmoja wao na uhakika wake kwa mujibu wa mtizamo wa Uislamu. Rai, fikra na sheria zinazo linganiwa na mfumo huo na kuupima mujama upo katika hali gani na ni rai, fikra na sheria zipi ambazo zime athiri mujatama. Na kuja mabadiliko na marekebisho na ijtihadi (zinazo fanywa) na uhakika wa ijthadi hizi katika usuli (misingi) na furui (matawi). Na Je Uislamu unazikubali ijthaad hizo au hauzikubali kama vile vile inavyo tulazimu kujua hali ya nafsia ya Ummah (kujifunga na sheria za Kiislamu) katika muda ambao Ummah una shuhudia kwa macho yake vipi Shari'ah, rai na fikra za Kiislamu zinavyo zama katika dunia hii wanayoishi. Na kwa upande mwingine Ummah una shuhudia sheria zinazo tawalishwa na mfumo uliopo wa utawala kwa hongo, hadaa na upanga.

Pia ina tulazimu kujua muelekeo wa Ummah kwa jumla yake na vipi Ummah unavyo zichukulia hizi nidhamu zinazo tawalishwa juu yake ambazo zina utishia Uislamu wake, kuuondosha na kuuporomosha ndani ya shimo la maangamivu na mateso. Kisha kujua muelekeo wa mufakirina katika Ummah ni kwa kiwango gani wanavutiwa na mfumo huu wakifisadi unao tawalishwa juu yao. Na Je mfumo huu umewajenga kuwa na dharau na kujua ni kwa kiwango gani wameathiriwa na vishawishi au vitisho na vipi walivyo chotwa na vishawishi hivi au kutishwa na wakatishika .

Kisha kukijua kikundi chenyewe cha kichama, Je kinazo hisia za juu na komavu, fikra komavu za kindani na ikhlasi ya kweli. Na mambo yote yaliyopo katika mujtama hayaja dhoofisha imani yake juu ya Uislamu na Shari'ah zake na kwamba vishawishi, vitisho kufanyiwa ugaidi, hongo na mateso vyote hivyo havija kiathiri hata chembe, na kufanya umakinifu kwamba kikundi hichi kimehifadhi hadhi yake kidhati ukweli wa kuhifadhi. Na kwamba mazingira yake ya kiimani yapo salama na fikra za Kiislamu zimekita barabara na kutabani maslahi ya Ummah na kukubali kwake kubeba majukumu ya Ummah yote haya yawe kamilifu. Kiasi kwamba mfumo ulindwe iwe iwavyo dhulma, kamatakamata kufungwa mateso, kisha kuhakikisha kikundi hichi kipo imara katika azma yake na kuwa tayari kubeba majukumu yake ikiwa ni pamoja na kujua matokeo yanayoweza kuwafika wawe tayari kuyabeba.

Na uchambuzi juu ya hizi harakati katika historia na zilivyosasa, unatupatia uhakika juu ya kujua mwenendo wa chama cha kimfumo kwa kuzingatia kuwa ni harakati ya kikundi na kupata kujua kama kime timiza masharti yake na kina kwenda katika mwenendo wake wa kawaida ili ikionekana kuna mgando au ikionekana kuna hitajika kurekebishwa katika aina fulani ya masomo kitengo fulani (jihazi) au kuna mazoea katika uendeshaji wa mambo au kuna ugumu katika maingiliano basi zitatafutwa mbinu ambazo zitakazo wezesha kufikisha ujumbe kwa Ummah na zenye kuufanya Ummah uwe ni wenye kubeba ujumbe kuupeleka kwa Ummah zingine.

Na kikundi cha kimfumo kilicho sahihi kitakwenda kwa kufuata njia hii:

**1**. Kupatikane mtu mkomavo wa fikra na hisia aujue mfumo na avaane nao na kwake mwenyewe uwe wazi. Na iwe kwa kutoka hatua moja kwenda nyingine na mfumo kwake uwe wazi kabisa na fafanuzi. Hapo kihakika kutakuwa kumepatikana kiini cha mwanzo na kiini hichi hakito chukua muda mrefu kitaanza kuonegezeka japo itakuwa ni kwa uzito basi

watapatikana watu wengine ambao na wao watakuwa ni viini na wao wataanza kuingiliana na wengine kwa malengo ya kimfumo basi halaqa ya mwanzo itaanzia kwao yenye malengo ya chama cha kimfumo (watarajiwa wao kuwa ndio viongozi wa chama) na mfumo pekee lazima uwe ndio lengo pekee la wao kuungana kwao pamoja na mfumo tu ndio liwe jambo pekee lililo washawishi kuvutika kwenye kundi.

**2**. Halaqa hii ya mwanzo kawaida yatarajiwa kuwa ni idadi kidogo na mwanzoni michakato yake itakuwa na uzito kwani hata kama ina zungumza mambo ambayo ndio hisia za mujtama inaoishi nao lakini maelezo yake na matamshi ambayo yenye kutofautiana na yale yaliyo zoeleka katika mujtama kuyasikia katika maneno na maana ya maneo

Na wao halaqa ya mwanzo watakuwa naufahamu mpya wenye kutofautiana na ufahamu ulioenea katika mujtama licha ya kwamba halaqa hiyo ya mwanzo itakuwa ina zungumza mambo ambayo ndio hisia za mujtamai hivyo halaka hii itakuwa kana kwamba ni ngeni katika mujtama na mwanzoni watu hawato vutika nayo kwa wingi ispokuwa wale tu wenye uwezo wa juu wa hisia mpaka itakapo patikana mazingira ya kuvutia watu kawaida kwenye smaku ya mfumo ambao umesha kita kwenye mwili wa halaqa hiyo ya mwanzo.

**3**. Uwezo wa kufikiri wa halaqa hii ya mwanzo watarajiwa ndio halaqa ya kiuongozi ni uwezo wa mkubwa sana na wa kindani, na njia yake (twariqa) ni ya kuelekea kwenye mabadiliko msingi yani mabadiliko yenye kuanzia mizizi basi halaqa hii ya mwanzo itaibuka ikiwa imezungukwa na mazingira mabovu ambayo ndio mujatama unayoishi nayo itapaa angani kiufahamu na itakuwa ukiona hali halisi (waqia) na pia ikiona waqia ambao inataka kuupeleka Ummah ili Ummah ukaishi katika hali hiyo mpya yaani inaona maisha mapya ambayo inataka kuuhamishia Ummah huko. Kama vile inavyona njia ambayo itapita ili kubadilisha waqia. Kwa mtindo huo halaqa hii inaona yaliyo nyuma ya ukuta katika hali ambayo mujtama mwisho wa kuona kwake ni mbele ya ukuta na kwa sababu za mujtama kugandamanana hali unaoishi basi inakuwa vigumu kunyanyuka juu kififkra. Hivyo basi, inakuwa ni vigumu kwa mujtama kufahamu kwa usahihi namna ya kubadilisha hali halisi. Kwani mujtama uliodorora, fikra kwake inakuwa katika hali ya uchanga na inategemezea kufikri kwake kwenye hali halisi kisha kupima mambo kipimo cha kimakosacha kijumla na kujipeleka kwa kufuata hali halisi hivyo hufanya manufaa yake yaburuzwe na kufuata hali ilivyo.

Ama halaqa ya mwanzo ya kichama yenyewe katika fikra zake inakuwa imeshavuka hali ya uchanga na kuelekea kwenye ukamilifu. Itafanya hali halisi ni sehemu (maudhui) ya kufikiria kufanyia mageuzi kwa kuufata mfumo na sio chanzo na msingi wa kufikiri na kuufanya mfumo ufate hali halisi basi itafanya kazi ya kuibadili hali halisi na kuilazimisha ifuate mfumo kama halaqa hiyo itakavyo na hatimaye hali halisi ifuate mfumo unao aminiwa na halaqa hiyo na sio kuufanya mfumo ufuate hali halisi kwa sababu hizi kutakuwa na pengo baina ya halaqa ya mwanzo ya chama na Ummah katikaufahamu wa mtazamo maishani na itahitaji kuzibwa kwa kuukurubisha Ummah katika ufahamu wa halaqa ya mwanzo ya chama.

**4**. Hakika fikra ya halaqa ya mwanzo (uongozi) imejitegemeza katika kanuni thabiti isiyo yumba nao ni fikra lazima iungane na vitendo na kwamba fikra na vitendo lazima viwe na lengo maalum linalo kusudiwa. Hivyo basi kwa kuwa halaqa ya mwanzo itakuwa hivi kutokana na kuvaana na mfumo na kutokana na kujitegemeza kwenye kanuni basi

kutapatikana mazingira safi ya kiimani yaliyo thabiti jambo ambalo litasaidia katika kulazimisha hali halisi na kuibadilisha. Kwani fikra hii haisukumwi na mambo yalivyo bali yenyewe ndio inasukuma mambo itakavyona hili ni tofauti kwa mujtama uliozorota kwani wenyewe fikra yake haina kanuni thabiti kwani kwa ujumla wake haujui malengo ambayo utafikiria kwa ajili yake na ufanye kazi kwa ajili ya kufikia lengo hilo bali malengo huwa ni kila mtu ana yake na ubinafsi. Hivyo basi hautokuwa na mazingira ya kiimani basi utalazimika kusombwa na yaliyo uzunguka mujtama na wala sio kugeuza hali na ifuate mujatama na kufikia hapo kutakuja mvutano mwanzoni baina ya halaqa ya mwanzo na mujtma ambao halaqa inaishi nao.

**5**. Ni wajibu kwa halaqa ya mwanzo (uongozi) ilete na kueneza mazingira ya kiimani kwa Ummah ambayo huletwa kwa njia ya kufikiri basi ni lazima iwe na mipango na mikakati ya makusudi kujikuza yenyewe tena kujikuza kwa haraka na kujisafisha kikweli kweli kiujenge mwili wake wa kichama ujenzi ulio salama na kwa haraka ya hali ya juu na kianze kusonga mbele kwa haraka na kufikia mabadiliko ya kutoka kuwa ni halaqa ya kichama na kuwa ni kundi la kichama kisha kuelekea kuwa chama kamili kitakacho jitosa ndani ya mujtama na kiwe ni chenye kuathiri mujtama na sio chenye kuathiriwa.

**6.** Harakati za makusudi zitafanyika kwa kuusoma Ummah kwa umakini na watu wake binafsi na mazingira huku kukichungwa kwa hadharikubwa kusipenye kiungo kibaya ili kusije patikana makosa katika uundwaji wa vitengo vyake ambavyo ndio tegemeo la chama ili chama kisije pelekwa kombo na kisije pasuka vipande.

**7**. Lazima aqida iliyokitana thabiti pamoja na thaqafa ya kichama ndio viwefungamano kwa wanachama na iwe kanuni ambayo kundi linayoifuata na si kanuni zilizoandikwa kwenye mafaili. Njia ya kukuza hii aqidana thaqafani kusoma na kufikiri ili akili ijengeke mjengeko maalumu na ili fikra ziungane na hisia. Ni lazima haya mazingira ya imani yadumu na yabakie ili kilindwe na kuhifadhiwa chama chote kupitia kuhifadhi mambo mawili: akili na moyo. Hivyo basi ni kiungo muhimu kuuamini mfumo ili moyo uweze kuanza kuwaunganisha wanachama wa chama. Pili kinacho unganisha chama ni akili, kutokana na kuusoma mfumo, kuuelewa na kuurudia. Kutokana na hayo ndio chama kitakuwa kimefanya maandalizi sahihi na fungamano lake litakuwa ni madhubuti lisilo yumba mbele ya misukosuko yote.

**8**. Halaqa ya chama ya mwanzo (uongozi) kwa njia moja au nyingine hufanana na mota ya kimashine na kwa njia nyingine hutofautiana

Ama upande wa kufanana nayo ni

Mfano mota ya kimashine ya gesi ina nishati ya joto linalo zalikana kutokana na plug (cheche) na mafuta. Mzunguko wa mota na nishati hii ya joto huzalisha msukumo (pressure) namsukumo huu huzungusha shafti nayo ndio inayo sukuma vitu vyote na hulazimika kuzunguka kwa sehemu zingine na chombo huanza kuzunguka hivyo basi kupatikana plug (cheche) na mafuta ndio chanzo kwani ndipo kukazalikana nishati ya joto nakukapatika msukumo na msukumo huu ndio ulio zungusha vitu vyote na mota ikaanza kuzunguka, na mota ikisita tu basi sehemu zote zina sita. Hivyo basi hakuna budi kupatikane plug (cheche) na mafuta na mzunguko wa kimota ili mota izunguke na sehemu

zote zizunguke ndivyo ilivyo halaqa ya mwanzo (uongozi). Fikra ni kama plug (cheche) na hisia walizo nazo watu wenye fikra katika uongozi ni sawa na mafuta na mtu ambaye hisia zake zina athirika na fikra zaka hiyo ni kama mchakato wa kimota basi fikra pale inapo kutana na hisia kwa mwanadamu huzalisha nishati ya joto basi huusukuma uongozi kufanya harakati. Harakati zake hizi zitaenea kwenye viungo vinginevya chama kuanzia mtu mmoja mmoja aliye ndani ya chama vitengo vyake na kamati zake na vingine vyote vitaathirika kwa joto lake navyo vitaanza kutaharaki. Hatimaye vyote vitaanza kuzunguka mzunguko wa kichama na hapa ndipo chama kitaanza harakati na kuanza kukuwa na kujipanga vizuri.

Basi ni lazima kueneza nishati ya joto kutoka kwa uongozi kwenda katika vitengo vingine vya chama mpaka mzunguko uanze ni kama vile kwa moto ya kimashine haizunguki mpaka kupatikane nishati ya joto na huu ndio upande wa kufanana kwake baina ya mota ya kimashine na baina ya uongozi wa chama. Basi ni lazima kwa viongozi wa chama kuwa makini na jambo hili na wafululize mawasiliano yao na harakati zao na vitengo vingine ili viathirike na joto la uongozi lienee kwenye vitengo vyote na uongozi utakapo fuatilia na kuwasaliana kwa mara kadhaa na ukaona kuwa bado kuna baadhi ya wanachama hawaja shika vizuri moto na kutaharaki basi wasikate tamaa na wajue kuwa hilo ni jambo la kutarajiwa kwani kifaa hakizunguki ila chombo chote kitakapo zunguka na kueneza joto kutoka kwake.

Ispokuwa uongozi wa halaqa ya mwanzo kuathiri kwake hakutokuwa ni kulazimisha katika chama kama mota inavyo lazimisha kwenye viungo vingine katika mota ya kimashine bali kusukuma kwake ni mwanzo tu. Ama baada ya chama kusonga mbele haiwi hivyo basi kwa upande huu uongozi wa chama una tofautiana na mota ya kimashine kwani mota ya kimashine yenyewe itaendelea kusukuma viungo. Lakini wanachama wa chama na vitengo vyake ni binadamu na sio chuma ndani yao kuna uhai na wataathirika kwa joto la uongozi yani joto la mfumo lita waathiri ambao umevaana na halaqa ya mwanzo ya kiuongozi. Hivyo basi baada ya wao kufahamu fikra na kuwa na mahusiano na uongozi wa kichama basi na wao wanakuwa ni sehemu katika mota. Hapo itakuwa ni harakaati ya kiuongozi kutokana na nishati ya joto inayo sambazwa kimaumbile katika chama chote kwani nayo ikiwa ni mota ya kijamii itakuwa fikra imetapakaa na kuenea kwenye chama chote hapo si uongozi tu ndio utabakia ukibeba harakati za kimota bali kwa kukuwa kwake na kukamilika kwake katika uundaji wa chama. Chama chote kitakuwa kimebeba harakati za kimota hapo basi kusonga mbele kwa chama hakuto hitajia uongozi wa halaqa ya mwanzo ya kichama na wala kusambaza joto bali mfumo utapelekwa na wanachama wa chama na vitengo vyake vitazunguka vyenyewe pamoja na halaqa zingine na kamati zake. Bila kuhitajia msukomo wa uongozi kwani joto latoka sehemu zote na kutoka kwa kila mwenye fikra mng'aavu katika chama na mwenye kuhusiana na vitengo hivi vyote mahusiano ya kawaida.

**9**. Chama cha kimfumo huenda hufuata hatua (marhalah) tatu mpaka kufikia kuutawalisha mfumo wake katika mujtama:

**Mwanzo:** kusomesha na kumakinisha thaqafah ya chama.

**Pili**: kuingiliana na mujtama tunaoishi nao mpaka mfumo uwe ni mazoea kwa mujtama (urfu aamu) yenye kutokana na ufahamu jumla (wai amm) wa jamii na jamii iuone kuwa

huo ni mfumo wake ili iweze kuuhami na kuutetea. Katika hatua hii kutaanza mivutano baina ya Ummah na wale wanao simama kuzuia mfumo usitawalishwe wakoloni na watawala vibaraka walio gizani na walio korogwa akili zao kwa thaqafa ya wakoloni walio wekwa mbele katika miji yetu kwani Ummah utakuwa umetambua kuwa mfumo huo ndio mfumo wake na kukitazama chama kuwa ni kiongozi wake.

**Tatu:** kuchukua hatamu za utawala kupitia kwa Ummah, kuchukua kikamilifu ili utawala uwe ndio njia ya kutawalisha mfumo kwa Ummah. Katika hatua hii chama kitaanza kazi za kivitendo katika maisha na kazi ya da'wah. Chama kitabakia na kuendelea kuulingania mfumo kwani mfumo ni ujumbe unao bebwa na Ummah na serikali.

**10**. Ama hatua ya kwanza ni ya kuasisi ni hatua ya kuwaangalia watu wote katika Ummah kama wasiokuwa na thaqafa sahihi ya kurudisha mfumo utawale. Hivyo basi kwanza humthaqafisha kila atakaye taka kuwa mwanchama katika chama kwa thaqafa ya chama. Na kuufanya mujtama wote ni shule ya chama mpaka ihitimishe watu kwa muda mchache kikundi ambacho kitakuwa na uwezo wa wa kuingiliana na jamii na kufanya nao mazungumzo ya mabadiliko ya kimfumo.

Licha ya kwamba inatakiwa ifahamike vyema kwamba huku kuthaqafisha sio sawa na kusomesha watu shuleni au madrasa na kuwa ipo tofauti kubwa sana na madraa au shule. Hivyo basi ni lazima halaqa za masomo ya thaqafa ziende kwa ufahamu kuwa mfumo ndiye mwalimu na kwamba elimu na thaqafaha inayo someshwa ni kwa ajili ya mfumo tu na yale yalazima katika maisha na yachukuliwe papo hapo kwa ajili ya matendo katika maisha.

Basi ni lazima thaqafa iwe ya matendo yani isomeshwe ili (mtu) akafanyie kazi maishani na ni lazima kuweka kizuizi kizito sana baina ya akili za wanachama na tabia ya kusoma bila kufanyia kazi ili kuzuia thaqafah ya hizb isije kuwa kama ile za madrasa za kielimu.

**11**. Chama ni kikundi kilichosimama juu ya fikra na twariqa yaani juu ya mfumo waliouamini wanachama wake. Chama huwa ni msimamizi juu ya fikra na hisia za mujtama kuipeleka katika harakati ya mwamko na kuulinda mujtama kutokana na kuporomoka kifikra na kihisia. Chama ni madrasa au shule ya Ummah ambapo husomeshwa thaqafa, kuandaliwa na kusukumwa katika mambo ya maisha ya kiulimwengu. Chama ndio madrasa au shule ya kikweli inayoweza kufikia hili, ilhali madrasa au shule nyingine haziwezi hata zikitofautika, zikiwa nyingi na kupanuka. Lakini kuna tofauti baina ya chama na madrasa au shule ambazo ni lazima zifahamike:

A. Madrasa au shule hata kama barnamiji yake itakuwa sahihi haiwezi kudhamini kuleta muamko wa Ummah bila ya kuwepo chama katika mujtama kikiwa kama mwalimu wa mujtama kwani madrasa maumbile yake hata iwe huru vipi lazima itafuata ratiba (aina ya wanafunzi, muda wamasomo, muda wa kuhitimu, kufeli au kupasi nk) hivyo ina simama katika mtindo binafsi nainajifunga na sifa binafsi. Hivyo basi inakosa sifa ya kuweza kwenda sambamba na yanayo ukabili mujtama hata kama ikihitajika ifanye. Hivyo basi itahijika muda mrefu na kazi ngumu ili iweze kujibadilisha. Zaidi ya hayo, maandalizi ya madrasa au shule yalivyo huwa ni maandalizi juu ya msingi wa kudumu usio badilika.

B. Chama kitakapo kuwa kimejengwa juu ya barnamiji ya sawa kitakuwa na haya yafuatayo:

1. Uhai: basi kitakuwa kina kuwa.
2. Kusonga mbele: hivyokitatoka hali moja kwenda nyingine.
3. Kufanya harakati: kitakuwa kina enea (na kueneza) maeno yote ya mujtama na kila sehemu katika miji yote.
4. Hisia: kitakuwa kina hisi na kupata hisia kwa kila kinacho ukumba mujtama na kuuathiri na kuandaliwa kwake (chama) ni maandalizi ya kuweza kwenda sambamba na hisia na hali halisi (kwa lengo la kubadilisha) basi chama kitakuwa na muda wote kinapiga hatua na kubadilika kwa kupata maendeleo na wala hakifuati mtindo wa ratiba kwani chenyewe kina kwenda sambamba na maisha yalivyo na mbadiliko yake ili kiyabadilishe maisha kwa kufuata mazingira ya kiimani na kuibadilisha hali halisi ifuate mfumo wa chama.

C. Madrasa au shule inafanya kazi ya kumpa thaqafa mtu binafsi kumlea na kumsomesha akiwa ni kama yeye mtu binafsi hata kama madrasa ni kama kijikundi kidogo lakini kwa upande wa usomeshaji wake ina somesha mtu binafasi. Hivyo basi matunda yake huwa ni ya mtu binafsi na sio ya wengi. Kwa mfano tukijaalia mji una wakaazi elfu kumi na kuna madrasa au shule zilizo kusanya wanafunzi elfu moja basi haziwezi kuleta muamko wowote kwa wakaazi hawa elfu kumi.

D. Kinyume na chama kina fanya kazi ya kulea kundi kwa sifa yake kama kundi moja pasi na kuchukulia ni mtu binafsi. Chama hakiwaangaliii kwa jicho la mtu binafsi hawa wanachama walio katika chama bali kina waangalia kwa jicho kuwa ni sehemu katika mujtama. Hivyo basi kina thaqafisha kwa jumla kama mujtama kwa lengo la kusuluhisha sehemu katika mujtama na sio mtu binafsi. Hivyo basi natija ya chama imekuwa ni ya mujtama na sio ya mtu binafsi. Mfano lau katika mji kuna wakaazi milioni moja na kikawepo chama chenye wanachama mia moja tu basi kutapatikana muamko katika mji huu jambo ambalo madrasa au shule haziwezi hata kama zitatoa nguvu aina gani na bidi kubwa kutumika muda mrefu na kuhitimisha wanafunzi wengi.

E. Madrasa au shule inafanya kazi ya kumuandaa mtu binafsi ili auathiri mujtama anaoishi nao na hali ya kuwa hawezi kuathiri mujtama labda sehemu kidogo sana kwani ana sehemu kidogo sana ya hisia za mabadiliko na muda huo huo yeye ni dhaifu wa fikra katika kuamsha Ummah.

F. Kinyume na chama kina fanya kazi ya kuandaa kundi ili limuathiri mtu binafsi. Hakika kundi linaweza kufanya hivyo kwani hisia zake ni zenye nguvu na zenye uwezo wa kuamsha fikra. Hivyo basi kumuathiri mtu binafsi ina kuwa kwa uwezo wa juu sana na kwa bidi ndogo na muda mfupi. Chama kinaweza kueneza muamko kwani kinacho amsha fikra ni hisia zitakapo ingiliana na fikra kutapatikana harakati za kimuamko.

Kwa ufupi chama na madrasa au shule vina tofautiana katika nukta tatu kuu:

1. Madrasa au shule inafuata ratiba na imefungika, lakini chama kinakuwa chenye mabadiliko ya kusonga mbele na hakifuati ratiba na kina uwezo wa kwenda sambamba na hali ilivyo ili kuibadilisha ifuate mazingira ya kiimani ya chama.

2. Hakika madrasa au shule ina mpatia thaqafa mtu binafsi ili auathiri mujtama basi natija yake huishia kuwa ya mtu binafsi lakini chama kinatoa thaqafa kwa jamii itakayo athiri mtu binafsi basi natija yake inakuwa ya kimujtama.

3. Madrasa au shule humpatia mtu binafsi sehemu ndogo sana ya hisia ili aweze kuathiri hisia za jamii basi huwa hawezi kuathiri na anashindwa kuuamsha Ummah. Lakini chama kina andaa kundi kihisia kamilifu ili kundi liweze kuathiri fikra za mtu binafsi basikundi litaweza kuathiri na lina uwezo wa kuamsha fikra uamshaji kamili.

**12.** Katika hatua hii ni lazima udumu ufahamu kwamba mujtama wote ni shule kubwa ya chama bila kusahau tofauti kubwa iiyopo baina ya chama na madrasa au shule.

Ama ukichukulia mujtama wote ni kama shule ya chama ni kwamba jukumu la chama katika kipindi hichi ni kuhakikisha kina eneza aqida safi na kuleta fahamu za sawa na hili halito wezekana ila kwa kutoa thaqafa na chama ndio kiwe mwalimu. Na thaqafa yake ndio masomo yanayo someshwa, mfumo huu pamoja na thaqafa hii vitakuwa vime jikita ndaniya mtu aliye uvaa huu mfumo basi wao ndio watakuwa maustadhi wa Ummah mubashara.

Na vitengo vyake na halaqa zake ndio safu zake na mujtma wote ni shule yake na jukumu hili la utoaji thaqafa lina lazimisha liwe kwa wanachama wa chama hicho na wawe wame tabanni fahamu zake kwa kusoma kindani na kufahamu ufahamu ulio sahihi na kwa kudurusi masomo ya kichama muda wote na kuhifadhi katiba yake na hukumu zake muhimu na kanuni msingi ambazo chama kime zitabbani. Na hilo lina hitaji kazi ya utoaji thaqafa kwa hali hiyo imekuwa ni lazima kuchunga suala la kusoma kwa kila anaye taka kujiunga pasi na kujali amesoma masomo ya chuo kikuu au ya msingi au ana onekana ni mtu mwenye uwezo wa kithaqafa. Uzembe wowote utakao fanyika kwa mtu yeyote juu ya hili basi mtu huyo atakuwa nje ya chama hata kama atajinasibisha na chama na huenda akasababisha madhara katika muundo jumla.

Lazima kuweka kizuizi kikubwa baina ya kazi na chama, katika kipindi hichi kabla chama hakija andaa watu walio iva kithaqafa ya kichama. Hivyo basi hatua hi imekuwa ni ya kutoa thaqafa na si zaidi. Ama kutambua kuwa kuna tofauti kubwa baina ya chama na madrasa au shule katika utoaji wa thaqafa hilo ni kwa lengo la kuzuia utoajii wa thaqafa ya chama usije geuka na kuwa kama wa madarsa au shule ili chama kisipoteze utendaji wake.

Basi lazima kuweka kizuizi kikubwa kwa wanao taka kuingia ndani ya chama na upande wa kielimu ya kimadrasa au kishule katika utoaji na upkeaji thaqafah ya kichama na izingatiwe kuwa thaqafa ya kichama lengo lake ni kubadilisha fahamu mbovu na kufanyia kazi maishani na ubebaji fikra kiongozi (qiyadat fikraya) kwa Ummah. Haitakiwi msomaji asome kwa malengo ya kielimu na kama atakuwa na haja ya elimu tu basi aende madrasa au shule na sio kwenye chama. Katika hatari ni kuelekea katika mtindo wa kimasomo na kuachana na misingi ya kichama kwani kutapoteza rutuba ya ufanyajikazi na itachelewesha kufikia hatua ifuatayo katika hatua zake.

**13**. Hatua ya pili ni ya kuingiliana na Ummah na hii huenda sambamba na mivutano. Ina zingatiwa ni hatua muhimu sana.Kufanikiwa kwake ni dalili ya kufanikiwa hatua ya uundwaji wa chama na kufeli kwake ni dalili kwamba kuna makosam yanayo hitaji kurekebishwa na yanatokana na makosa ya nyuma. Hivyo basi sharti la kufanikiwa hatua ya pili lipo kwenye kufanikiwa hatua ya kwanza.

Lakini kufanikiwa katika hatua ya mwanzo pekee haitoshelezi katika kufanikiwa katika hatua hii ya pili. Bali lazima kufaulu kithaqafa na kujulikaniwe na watu yaani watu wajue kuwa kuna da'awah na wamjue mwanachama kuwa ana beba da'wah. Kama vile ambavyo roho ya kipamoja iwe imesha tengenezwa wakati wa utoaji wa thaqafa katika halaqah na kwa kuwasilina wan chama na jamii wanayoishi nayo na bidiizao za kutaka kuathiri mujtama hata watakapo hamia hatua ya pili basi maandalizi ya mujtama yanakuwa yapo tayari hivyo inakuwa rahisi kuingiliana na Ummah.

**14.** Mwanachama wa chama asiingie katika dori ya kuingiliana na Ummah kabla ya dori ya thaqafa na baada ya kuwa kishaiva kithaqafa. Uivaji ambao umemjenga kuwa na shakhsiyya ya Kiislamu inarandana na aqliyyah na nafsiyya yake. Amesema Mtume (saw):

***"Hatokuwa na Imani mmoja wenu mpaka matamanio yake yawe kwa yale niliyo kuja nayo"***

Pamoja na kuiva kithaqafa lazima watu wamjue kuwa yeye ana beba da'wah ya Kiislam. Muelekeo wake wa kipamoja kwa kuwa ndani ya kundi uwe umeimarika na upo wazi kwa kuhudhuria kwake kwenye halaqa na kwa kuingiliana kwake na mujtama kiasi kwamba hali ya kujitenga itakuwa imesha ondoka. Tabia ya kujitenga ni mchanganyiko wa uoga na kukata tamaa na hili ni lazima ling'olewe kwa watu binafsi na mujtama.

**15.** Chama kitahama kutoka dori ya thaqafa na kuelekea dori ya kuingiliana na Ummah kimaumbile. Lau kita taka kuingia dori ya pili kabla ya muda wake kitashindwa. Kwani dori ya thaqafa ndio hukamilika hatua za kuanzia. Thaqafa ndio itafanya mfumo uvaane na wanachama na ndio inafanya mujtama uhisi kuna da'wah kuhisi kwa wazi kabisa yaani mfumo upandikizwe katika vifua vyao wanachama na mujtama. Kupatikana hisia kwa mujtama na muda wowote itakapo timia kuvaana na mfumo yaani kuupandikiza mfumo katika nafsi zao na ikatimia kwa mujtama juu ya mfumo. Hivyo basi da'wah inakuwa imevuka hatua ya kiawali na inakuwa hakuna bodi kuingia hatua ya kusonga mbele.

Chama ili kianze kuingia katika hatua ya kusonga mbele basi lazima kianze kuuzungumzisha Ummah. Ili kiweze kuuzungumzisha Ummah basi hakuna budi kianze majaribio mpaka kitakapo faulu majaribio yake haya. Hivyo basi kitaanza rasmi kuuzungumzisha Ummah moja kwa moja. Majaribio ya kuuzungumzisha Ummah ni kwa kutoa thaqafa masomo ya halaqa yaliyo na umakini na kwa kutoa thaqafa ya pamoja kwa kwa watu wengi katika maeneo yote yanayo wezekana, na kwa kufichua mbinu za kikoloni na kutabanni maslahi ya Ummah. Na kitakapo fanikiwa katika mambo haya manne basi na kitahamia hatua ya kusonga mbele (hatua ya pili) kimaumbile. Itakuwa kuhamia kwake kwenda hatua ya kusonga mbele ndicho kinacho kihamisha chama uhamaji wa kimaumbile kutoka hatua ya kwanza ambayo ni dori ya thaqafa kisha kuingia marhala ya pili ambayo ndio dori ya maingiliano na kitafanya kuanza kuingiliana na Ummah ni jambo kimaumbile.

**16**. Na kuingiliana(interaction) na Ummah ni jambo la lazima ili chama kifaulu katika kazi yake, kwani wanachama hata wawe wengi kiasi gani wasipo ingiliana na Ummah hawato weza kuifanya kazi hii wakiwa peke yao hata wawe na nguvu kiasi gani. Isipokuwa mpaka Ummah utakapo kwenda pamoja nao na wala hawatoweza kuushawishi Ummah kushiriki kazi hii na hawato kuwa pamoja ila tu watakapo ingiliana nao na wakafanikiwa katika

maigiliano haya. Haimaanishi kuwa kufanikiwa kuingiliana na Ummah ni kuwakusanya wote ndaniya chama kwa pamoja bali makusudio ya kuingiliana na Ummah ni kuufahamisha Ummah mfumo wa chama ili Ummah uuchukue huo mfumo na kuufanya kuwa wake. Kwani kiasili mfumo huu ni wa Ummah kwani ni Uislamu, na upo kwa Ummah. Kilichobadilika ni kuwa sasa hisia za Ummah zimegeuka kuwa kutoka kuwa ni hisia kavu kavu na kugeuka na kuwa fikra na zikapambanuka kwa kikundi fulani chenye ukomavu wa juu wa ufahamu) na chama kikaundwa kutoka kwenye kikundi hich. Kanuni msingi ya hisia hizi ikawa ni ***fikra na utendaji viwe kwa malengo kusudiwa*** kielelezo kiwakilishi cha kweli juu ya mfumo. Hivyo utakuwa mfumo yaani Uislamu ndio hisia za kindani za Ummah na chama kinakuwa msemaji wa hisia hizi. Hivyo basi ikiwa chama kitakuwa fasaha katika maelezo lugha ya wazi yenye kufahamika na watu wote, chenye maneno ya kweli basi Ummah utaufahamu mfumo kwa haraka sana na Ummah utaingiliana na chama. Na Ummah wote utahisabika ni kama chama na kile kikundi maalum kitafanya kazi ya kiuongozi wa kiharakati wa kichama. Zitafanyika harakati na Ummah za kuelekea kwenye hatua ya tatu chini ya uongozi wa chama. Hatua ya kutawalisha Uislamu utawalishaji kamili wa kimapinduzi kwa kuzingatia kuwa hiyo ndio njia pekee ya kutekeleza fikra yaani kwa kuzingatia kuwa ni sehemu katika mfumo.

Lakini kuna vikwazo kadhaa wa kadhaa vinavyo simama mbele ya maingiliano haya. Ni lazima kuvijua na kuvijua maumbile yake ili ifanyike kazi ya kuvishinda na vikwazo hivi ni vingi lakini vya muhimu ni hivi:

A. ***Mgongano baina ya mfumo na nidhamu inayo tawala mujtama***

Hakika mfumo wa chama ni nidhamu mpya ya maisha na litakuwa ni jambo geni kwa mujibu wa mujtama ulivyo. Mfumo (Uislamu) uta gongana na nidhamu inayo utawala mujtama na ni kundi la watu wachache (mabepari) ndio wanatawala wetu wengi. Hivyo basi kundi dogo hilo litaona kuna hatari kubwa juu yao kutokana na mfumo huu mpya wa Kiislamu na juu ya tawala zake. Hivyo lazima litasimama mbele yake na kupiga vita kwa kila aina ya mbinu mfano Uvumi (propaganda), kuwaandama wabebaji da'wah na kwa kutumia mbinu na vyombo vya kisiasa.

Hivyo basi ni lazima kwa wabebaji da’wah kujilinda na madhara huku wakiendelea kuingiliana na Ummah kwa kuwaita kwenye mfumo wake – na wavumilie maudhi kwa kila watakavyo weza na kukabiliana na uvumi na propaganda zenye kupotosha, iwe ni kwa kufafanua da''wah ya chama chake na wawe tayari kuvumilia kila aina ya mateso katika njia hii.

B. ***Na miongoni mwa vikwazo ni kuwepo kwa thaqafa zenye kutofautina***.

Pamoja na kuwepo fikra tofauti tofauti katika Ummah, pia kunazo thaqafa tofauti katika mujtama. Lakini Ummah una hisia moja. Thaqafa tofauti hususan zile za kikoloni ambazo zitakuwa zina wakilisha mitizamo yenye kuzigeuza hisia hizi katika muda ambao thaqafa ya mfumo yaani wa Kiislamu ina wakilisha hisia za kweli za Ummah. Isipokuwa rai jumla ya Ummah (rai amm) ya thaqafa ya mujtama na mitaala ya elimu shuleni na vyuoni na sehemu zote za kielimu zitakuwa zina kwenda sambamba na thaqafa ya kikoloni na pia harakati za kisiasa na kithaqafa zitakuwa zinakwenda kwa kufuata thaqafa ya kikoloni. Hivyo basi, hakuna budi kwa chama katika kufikisha thaqafa kuingia katika mgongano wa

kithaqafa na kifikra mpaka kishinde na kiweze kuziwakilisha kwa usahihi hisia na fikra za Ummah ili Ummah uende sambamba na chama.

Na kufikia hapa itakuwa ni lazima katika hatua hii kupatikane mgongano baina ya thaqafa na fikra za chama dhidi ya thaqafa na fikra zilizoenea katika mujtama na mvutano huu utakuwa baina ya Waislamu kwa Waislamu. Hivyo kusifanyike mijadala yenye kupoteza muda. Bali wanachama wa kundi waendelee kufuata njia yake iliyo nyooka ili kuweka sawa njia zilizopinda. Na katu wasijitumbukize kwenye mijadala tasa ili kuzuia kujenga chuki binafsi jambo ambalo hutia upofu na uziwi mtu kufuata haki hatakama baadaye itambainikia.

Lakini chama kifafanue na kuchambua fikra za chama na kibainishe makosa yaliyomo katika fikra zingine na ubatili uliomo ndani ya thaqafa zingine na hatari iliyomo ndani ya fikra hizo. Chama kikifanya hivyo Ummah utaachana na fikra hizo za kimakosa na utaelekea kwenye thaqafa ya chama na fikra zake bali hata wale wabebaji wa fikra hizo nao pia wataachana nazo baada ya kudhihirika upotofu wake kama watakuwa kweli ni wenye ikhlasi, ufahamu na wasafi wa nafsi. Hii ndio kazi kubwa zaidi katika chama.

Kuleta maingiliano na Ummah katika maeneo ambayo imekita mizizi ya thaqafa ya kikoloni inakuwa ni kazi kubwa zaidi kuliko maeneo ambayo haijakita sana. Na eneo ambalo wasomi wa thaqafa ya kikoloni wapo kwa kiwango cha chini ni wepesi kuwa na muamko wa kukubali mabadiliko kuliko maeneo ambayo kuna wasomi wengi walio athiriwa na thaqafa ya kikoloni. Hivyo ni lazima kwa chama kutambua kinafanya maingiliano na kundi la aina gani ili kiende sambamba na kundi hilo.

B. ***Na katika kikwazo kikubwa ni kuwepo kwa watu wenye kufuata hali halisi***

Na hili ni baada ya kuwepo kwa thaqafa ya kikoloni, sumu za kikoloni na ujinga kukapatikana makundi mawili yenye kufuata fikra za hali halisi.

***Kundi la kwanza; Hili ni kundi la kufuata hali halisi***

Ni watu wanaofuata hali halisi na kuridhia na hali halisi na kusalimu amri mbele ya hali halisi kwa kila jambo; kwani kundi hili limefanya hali halisi ndio chimbuko la wao kufikiri na suluhisho la matatizo wanachukua kufuata hali halisi.

Na njia ya kulishinda kundi hili ni kuzama nao kiundani katika chambuzi mbalimbali mpaka waone kuwa hali halisi hufanywa ni maudhui ya kufikirina sio msingi wa kuchukua fikra. Hivyo basi, wanaweza kuachana na fikra hizo (hawa ni mfano wa wasomi)

***Kundi la pili: Ni kundi la gizani (stagnation) ambalo halitaki kuishi kwenye nuru***

Ni watu walio zoea maisha ya gizani na wamezoea mambo duni ya ovyo na kusibiwa na maradhi ya uvivu na uzembe kiakili na kimwili. Watu waliogandamana na mambo ya kale kutoka kwa mababu kwa sababu tu ni ya kale. Hivyo basi, hawa ndio hasa wenye kufuata hali halisi kwa kuwa hawataki mabadiliko na wao wamekuwa ni sehemu ya hiyo hali halisi na wameganda kifikra. Hawa wana hitaji nguvu na juhudi za ziada na njia ya kuwashinda watu hawa ni kuwasomesha kithaqafa na kutumia juhudi za juu katika kurekebisha fahamu zao (hawa ni mfano wa watawala na wapambe wao).

**D.** ***Na katika vikwazo vilivyopo mbele ya dawa ni watu kufungamana na maslahi yao.***

Mwanadamu hujifunga na maslahi yake binafsi na shughuli zake za kila siku lakini katika muda huo huo anajifanga na maslahi ya mfumo (Uislamu). Na huenda akaona kuwa maslahi yake yana gongana na da’wah ya mfumo hivyo ataanza kufanya juhudi za kuoanisha baina yake. Ili kushinda kikwazo hichi ni lazima kwa kila atakaye kinai na kuamini mfumo, afanye na ajue kuwa da’wah na chama ndio vinavyo panga maslahi yake binafsi (atangulize da'wah kabla ya kazi zake) haikubaliki kufanya kazi ambayo ina gongana na da’wah au itamfanya ashindwe kubeba da’wa na kumsahaulisha na kumtilia vikwazo. Akifanya hivyo atakuwa ameipa da'wah nafasi yake nayo ni kufuata maslahi ya da'wah na mzunguko wake na sio da'wah ifuate maslahi yake na mzunguko wake binafsi kama mbebaji da'wah.

**E.** ***Kikwazo chengine kinacho ikabili da'wah ni jambo la kujitolea kwa mambo ya kidunia mali biashara na mfano wa hayo katika ubebaji da’wah na Uislamu***

Nakukishinda kikwazo hichi ni muumini akumbushwe kuwa Mwenyezi Mungu amenunua kwa waumini nafsi zao na mali zao kwamba watapata pepo. Na inatosha kwake ukumbosho huu na ana achiwa khiyari yake mwenyewe katika kujitolea kwenye mambo haya na wala asilazimishwe chochote. Mtume (ra) alimwandikia barua Abdallah bin Jahsh (ra) alipomtuma kwenda kufuatilia habari za makuraishi kwenye mitende iliyo baina ya Makkah na Taif na katika barua hiyo kuliandikwa: "***Usimlazimishe yeyote miongoni mwa uliofuatana nao, na nenda kwa amri yangu pamoja na watakao kufuata***"

**F.** ***Huenda ikadhaniwa kuwa katika vikwazo ni miji kutofautiana kimaendeleo***

Ummah ulivyo mijini sivyo unavyo kuwa vijijini na pia ni tofauti na mashambani. Maendeleo ya kimiji yaliyopo mjini sio yanayo kuwepo vijijini na pia sio sawa na yale ya mashambani au kwenye makambi ya mahema. Hivyo basi, tofauti hizi za kimaendeleo ya kimiji zinaweza kufanya chama kufikiri kutofautisha katika utoaji wa thaqafa au katika misimamo ya kimfumo au ufafanuzi wake. Hili ndio jambo hatari sana kwani Ummah uwe utakavyo kuwa hata kama watatofautiana katika munoekano wa kimiji lakini ni Ummah Mmoja na hisia zake ni moja na mfumo wake ni mmoja basi da'wah iwe moja tu.

**17.** Chama kitakapo fikia hatua hii ya (kuingiliana na Ummah) kitakabiliwa na hatari mbili:

Hatari ya kimfumo (yaani kwenye mfumo wenyewe) na hatari ya utabaka.

Hatari ya kimfumo ni kutoka kwa jamii hii italetwa na mihemko ya jamii katika hali ya kutaka kupata matakwa yeke na hili litakuja baada ya rai ya chama kuwajuu na kuzishinda rai zingine lakini jami itakuwa bado na mabaki ya fikra za kimakosa.

Nalo hilo ni pale chama kitakapo fanya kazikatika mujtama na kuwasiliana nawatu wengi na kuingiliana nao kwa lengo la kuchukua uongoz. Na muda huo chama kitakuwa kimejizatiti kwa mfumo wake lakini mujtama ambao utakuwa umekipenda chama wao wana fikra mkorogeko za nyuma, na mawazo ya kurithi toka vizazi vya nyuma, na athari ya fikra za kikoloni mbaya na athari ya kumuiga mkoloni. Hivyo basi, chama kitakapo simama na kufanya kazi ya kuingiliana na Ummah na kuingizia Ummah rai za chama na fikra zake na kikafanya bidii ya juu kuusahihisha Ummah fahamu zake na kueneza aqida ya Kiislamu na kutengeneza mazingira ya ukweli na mazoea (urfu amm) mazuri kwa kuathiriwa na fahamu

za chama. Hili lina hitaji ulinganizi na kampeni mpaka Ummah uunge mkono chama kwa msingi wa mfumo kiasi cha Ummah kuwa na imani juu ya mfumo pamoja na kuziamini fahamu za chama, kukihishimu na kuwa tayari kukitii na kufanya nacho kazi.

Hapo kazi ya chama itakuwa ni kuzidisha idadi ya wanachama ambao ndio wenye kukubalika kwa Ummah ili waendelee kushikilia hatamu kama vile afisa wa jeshi. Chama kitakapo faulu katika hatua hii ya maingiliano kita uongoza Ummah kuelekea kwenye malengo kinayo yataka ndani ya mipaka ya mfumo na hakito toka ndani ya mstari.

Lakini kitakapo ongoza watu kabla ya kukamilika hatua ya maingiliano na kabla hakija upatia Ummah ufahamu jumla (wai amm) basi uongozi wake utakuwa sio kwa kufuata hukmu na fikra za mfumo bali ni kwa kuyapigia debe mawazo na hisia za watakavyo Ummah na si utakavyo mfumo na kwa kuziamsha hisia zao na kuonesha kana kwamba wanayo yataka ni kesho tu watayapata na yapo mikononi mwa chama.

Isipokuwa watu hawa katika kipindi hichi cha kuvutiwa na chama hazito potea kabisa baadhi ya hisia zao za zamani kama vile utaifa, uqaumiya, na fikra za kiroho bila ya siasa na maisha na hali hizi zitakuwa zinaibuka baina yao na kutazuka fikra chafu za ubaguzi duni na mbovu kama za kimadhhabi na fikra za zamani kama kudai uhuru na mawazo ya usisi, u'asabiya, na utukufu wa familia. Hivyo basi kutazuka mgongano baina yao na baina ya chama kwani watu watakuwa wanataka mambo ambayo haya afikiani na mfumo wa chama na watu hawa watakuwa wanalingania mambo ya ubinafsi ambayo ndio yenye kudhuru Ummah lakini wao ndio watakuwa wana hamasika nayo na zogo na kelele zitakuwa ni kutaka matakwa yao yatimie. Na kutazuka kila aina ya ubaguzi hali ikifikia hapo chama kitakuwa baina ya makaa mawili ya moto:

Ima kuchukiwa na Ummah na kutupwa na kupoteza ushawishi wao walio ujenga au watupe na kuachana na misimamo yao ya kimfumo na kuanza kulegeza misimamo na yote haya mawili ni hatari kwa chama. Na iwe wazi kwa wanachama kwamba kunapo tokea mgongano baina ya Ummah na mfumo basi wao washikamane na mfumo. Wachukiwe na Ummah watakavyo chukiwa kwani hizi ni hasira za muda na wakiendelea kuwa na misimamo yao juu ya mfumo wataweza kurudisha imani ya Ummah kwao. Na wajihadhari na kuutupa mfumo kwa sababu ya Ummah na kupoteza dhati yake hata tembe kwani huo mfumo ndio uhai wa chama na dhamana pekee ya kufanya chama kiendelee kuwepo na hakuna njia ya kuweza kukwepa katika kipindi hichi kigumu.

Na ili kuondosha hatari hii basi ni lazima juu ya chama kufanya bidii kuukinaisha Ummah kwa fikra za mfumo wake na kuwa makini juu ya ufafanuzi wa fikra na fahamau zake uwe wazi kabisa na kufanya kazi ya kuhakikisha mazingira ya kuufanya Ummah uwe chini ya chama ni endelevu. Hilo jukumu lita rahisishwa kwa kutoa bidii za hali ya juu katika kusomesha na kuweka umuhimu mkubwa katika kutoa thaqafa kwa jumla jamala na kuongeza juhudi katika kukashifu mbinu za kikoloni ukosoaji kwa uhodari wa hali ya juu na kuendeleza kampeni hiyo kwa Ummah. Na kufafanua maslahi yake na kukiyeyusha chama na mfumo na kuwa kitu kimoja. Na kuwa makini na mchujo wa fikra za chama na fahamu zake ili kibakie kuwa safi na kutoa juhudi kadri iwezekanavyo kwa gharama yoyote ile ya nguvu na machovu itakayo tumika.

Ama hatari ya kiutabaka hili lisipo dhibitiwa hujipenyeza kwa wanachama na sio kwa Ummah na hili huzuka pale chama kitakapo kuwa ndio msemaji mkuu wa Ummah na kikawa ndicho chenye hadhi na kuheshimiwa na sehemu kubwa ya watu wakakipatia heshima kuanzia watu maalumu mpaka watu wote. Hali hii inaweza kuletea majivuno kwa hawa wanachama wakawa wanajiona wao ni wenye thamani kuliko watu wote na kwamba sasa wao kazi yao ni uongozi tu na Ummah wao kazi yao ni kufuata tu.

Hapo watajinyanyua na kujiweka juu ya Ummah bali hata wao kwa wao bila kujali ubaya wasuala hilo hali hiyo ikiendelea Ummah utaona kuwa chama ni tabaka jingine. Na kwa upande wa chama nacho pia kitakuwa kinajiona ni tabaka jingine. Na kuwepo hisia hizi ndio chanzo cha kuporomoka kwa chama. Kwani chama kitawabeza watu wa kawaida na watu wa kawaida watakibeza chama hapo Ummah utaanza kujitenga mbali na chama na Ummah utakapo kikimbia chama basi chama kimeporomoka. Na kitahitajia juhudi kubwa sana na yaziada ili kurudisha imani ya Ummah juu ya chama.

Hivyo basi ni wajibu kwa wafuasi wa chama wawe sawa na watu wa kawaida na wasijione ispokuwa ni watumishi wa Ummah na nafasi yao katika chama ni ya kuhudumia Ummah kwani wakiwa hivi ndio kinga yao. Na itawafaa si tu Ummah kuendelea kuwa na imani nao bali hata watakapo fikia hatua ya tatu watakapo kuwa wapo madarakani wakiufanyia kazi mfumo kivitendo wataendelea kuwa japo ni watala ni watumishi wa Ummah ili iwe kwao wepesi kuutawalisha mfumo.

**18.** Hatua ya tatu ni ya kuufikia utawala.

Hakika chama huufikia utawala kupitia Ummah kwa kufanya kazi ya kuomba nusra na utatekelezwa mfumo kwa mpigo au wote na kwa mara moja na hii ndio iitwayo *njia ya kimapinduzi* na njia hii haikubali kushiriki katika utawala nusu nusu bali ni kuchukua utawala wote na kuufanya utawala ndio njia ya kuutawalisha mfumo na sio malengo ya mwisho na wala haikubaliki njia ya utekelezwaji wa polepole (tajadurruj) vyovyote iwavyo.

Na mfumo utakapo tawalishwa kikamilifu basi itakuwa ni lazima ibebwe da'wah ya Kiislamu na dola itaweka katika bajeti yake mlango maalumu wa ulinganizi na propaganda. Na usimamizi huu wa da'wah utasimamiwa na upande wa serikali au chama kutokana na hali zitakavyo ruhusu. Licha ya chama kupata serikali lakini chama kitaendele kubakia na vitengo vyake vitaendelea kuwepo sawa wanachama wake wawe madarakani au hawako madarakani. Na serikali ina chukuliwa ndio hatua ya mwanzo kabisa ya kuanza kazi ya utekelezaji wa mfumo kivitendo na kisha kwenda mbio ili kuutawalisha kila kona ya ulimwengu.

Hizi ndizo hatua ambazo chama kitazifuata katika maisha ili kuihamisha fikra kutoka kuwa ni fikra mpaka kutekelezwa kivitendo na kwa lugha nyingine kuuchukua mfumo kutoka kuwepo vitabuni au akili tu mpaka kutawalishwa maishani nako ni kwa kurudisha maisha ya Kiislamu na kuunyanyua mujtama na kuibeba da'wah kuipeleka ulimwenguni kote na hapo ndipo chama kitakuwa kimeanza hatua za utekelezaji kivitendo. Na hilo ndilo lengo lilo fanya kuasisiwa kwa chama.

Kwa hivyo basi chama ndio dhamana pekeeya kusimama kwa dola ya Kiislamu. Kudumu kwake, kuutawalisha Uislamu ulimwenguni, na kuhakikisha unatawalishwa vizuri na kudumu kutawalishwa vizuri na kuibeba da'wah ya Kiislamu ulimwenguni kwani chama

baada ya kusimamisha dola kitakuwa mlinzi wa dola hiyo chenye kuihisabu (kuiwajibisha) na chenye kuuongoza Ummah kuijadili serikali utendaji wake na muda huo huo chama kitakuwa ni chenye kubeba da'wah katika miji ya Kiislamu na sehemu zote duniani.